

Jumatano Septemba 4, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581789
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**MAN UNITED YAMKINGIA KIFUA TEN HAG**

UKURASA 22

**Waziri** aagiza mwendokasi 670 Mbagala na Kimara

UKURASA 3



**Muswada** Sheria Hadhi Maalum kwa Diaspora waondolewa bungeni

UKURASA 2



**Kibano** chaja kwa wasioweka bei za bidhaa zao dukani

UKURASA 3

## PENDEKEZO UWT...

# Wabakaji wahasiwe, wanasheria waguna

UKURASA 2




"Sheria iliyopo sasa ya makosa ya jinai, adhabu zake zimeonekana hazitoshi kukomesha matukio haya nchini."

Subira Mgalu

"Hatubadili sheria kwa hasira au mihemko, vinginevyo tutakuja kutaka wanaobaka na wao wabakwe. Sheria lazima izingatie ustaarabu pia."

Boniface Mwabukusi



Rais Samia Suluhu Hassan akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Beijing Capital, China jana kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC). **PICHA: IKULU**

**UTUMBO NJE**



## Muhimbili yapokea watoto 7 kila wiki

UKURASA 5

## Uchaguzi wa Serikali za Mitaa njiapanda

UK. 2

**MICHEZO** **ATEBA: NITAFUNGA SANA MABAO SIMBA** UK.24 **MAONI,** UK.6

HABARI KITAIFA

# UWT wataka sheria ya kuhasi wanaume wabakaji, walawiti

**Paul Mabeja na Renatha Msungu,** DODOMA

UMOJA wa Wanawake wa Chama Cha Mpinduzi (UWT) umeomba serikali kutunga sheria ya ukatili wa kijinsia itakayobana wanaume wanaobaka na kulawiti kwa kuhasi wanaotiwa hatiani.

Umoja huo una mtazamo kwamba sheria iliyopo sasa ya makosa ya jinai, adhabu zake zimeonekana hazitoshi kukomesha matukio hayo nchini.

Ombi la UWT linakuja baada ya tukio la juzi saa tatu usiku la Damas Stephano, mkazi wa Mtaa wa Mbuyuni, Kata ya Kizota, jijini Dodoma, kudaiwa kunajisi na kulawiti mtoto wake mwenye umri wa miezi sita na kusababisha kufariki dunia.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya UWT Taifa, Subira Mgalu ambaye pia ni Katibu wa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisema matukio hayo katika jamii yamekuwa mengi nchini.

"Tunaomba serikali kutunga sheria ya masuala haya ya ukatili wa kijinsia, ili kutoa adhabu ya wanaume wanaobainika kulawiti ama kunajisi watoto wanahasiwa ili kukomesha hali hii na kuwa fundisho kwa wengine. Kwa sasa hali imekuwa mbaya zaidi," alisema Subira.

Mwili wa mtoto huyo anayedaiwa kunajisiwa hadi kufariki dunia na baba yake mzazi, ulitarajiwa kuzikwa katika makaburi ya Hijra jijini Dodoma jana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, alisema juzi kuwa wanamshikilia Stephano anayetuhumiwa kumlawiti hadi kufa mtoto huyo.

"Mtoto huyo amefariki (dunia) wakati akipatiwa matibabu kutokana na maumivu makali aliyopata kutokana na kulawitiwa na baba yake mzazi.

"Mtuhumiwa baada ya tukio lile alijificha kutokana na hofu ya kile alichofanya - kumlawiti mtoto wake wa miezi sita hadi kumuua, aliamua kukimbia, ili kukwepa mkono wa sheria lakini jeshi lilifanikiwa kumnasa na sasa uchunguzi unaendelea ili kumfikisha mahakamani kwa ajili ya kujibu tuhuma hizo," alisema.

**RAIS TLS**

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Boniface Mwabukusi, akizungumzia mtazamo huo wa UWT, alisema jana kuwa sheria zilizopo nchini ni kali na zinafaa kuendelea kutumika wakati huu.

Mwabukusi alisema kinachotakiwa kusisitizwa ni wahusika katika kesi hizo za ukatili kutekeleza wajibu wao ipasavyo ili kutoa haki kwa waathirika kwa wakati.

"Sheria tulizonazo nchini bado zinatosha kabisa na ni kali, sema kinachotakiwa ni wahusika kusimamia kwa maana ya mahakimu, waendesha mashtaka pamoja na watu wote wanaopaswa kutoa ushahidi, wautoe ili hukumu zipatikane kwa wakati.

"Maoni yanayotolewa na watu mbalimbali kuhusu kubadilishwa kwa sheria ya ukatili wa kijinsia ili wanaume watakaobainika kulawiti watoto wahasiwe, sheria lazima izingatie mambo muhimu. Kama unataka kubadili sheria, unataka kupata nini?

"Na hatubadili sheria kwa hasira au mihemko, vinginevyo tutakuja kutaka wanaobaka na wao wabakwe. Sheria lazima izingitie ustaarabu pia," alisema.

Wakili Mwabukusi alisema vitendo hivyo vya ulawiti wa watoto vinaumiza, lakini lazima sheria zizingatie ustaarabu kwenye jamii na si kuongozwa na hasira za watu.



Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo(wa pili kulia), Wakili Jebra Kambole (kulia), Wakili Dickson Matata (wa tatu kulia), Wakili wa Serikali, Erigh Rumisha (kushoto) na Wakili Mpare Mpoki (aliyekaa), wakifurahia jambo kabla ya kuanza kusikilizwa kwa kesi iliyofunguliwa na Jukwaa la Katiba ya kupinga TAMISEMI kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Uchaguzi wa Serikali za Mitaa njiapanda

**Na Grace Gurisha**

UCHAGUZI wa Serikali za Mitaa uko njiapanda: Wanaharakati watatu waliofungua kesi ya kikatiba kuzuia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuusimamia, wameomba mahakama itoe zuio la mchakato wake unaoendelea hivi sasa.

Kwa upande wake serikali, imetoa angalizo kuwa iwapo mahakama itatoa amri hiyo, wananchi watakosa haki yao ya msingi ya kidemokrasia ya kupiga kura.

Hoja hizo ziliwasilishwa jana mbele ya Jaji Wilfred Dyansobera wa Mahakama Kuu Masjala Kuu Dar es Salaam na jopo la mawakili wa upande wa serikali na waleta maombi ambazo zilichukua zaidi ya saa sita, jaji akihitimisha uamuzi utatolewa Jumatatu ijayo.

Akitoa hoja za kupinga mapingamizi ya awali ya Upande wa Serikali, Wakili Mpare Mpoki anayewawakilisha Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, Bubelwa Kaiza na Dk. Annanilea Nkya, aliiomba mahakama kutoa amri hiyo ili kuzuia kinachoendelea hivi sasa.

"Ombi letu limejikita katika kanuni ya tano na ya sita ya GN 324/2014, kama mahakama itatoa rukhsa, basi tunaomba itoe amri ya kusimamisha mwenendo wa uchaguzi huu kwa sababu waziri hana mamlaka hayo," alidai Mpoki.

Alidai kuwa Agosti 15, 2024, TAMISEMI ilitoa tangazo la uchaguzi huo, ambalo wameliambatanisha kwenye maombi yao, mchakato huu ulianza tarehe hiyo na utamalizika Novemba 27, 2024.

Akijibu hoja hiyo, Wakili wa Serikali Ayubu Sanga aliomba mahakama itoe uamuzi ambao hautaathiri upande wowote kwa kuzingatia sheria na kudai kuwa alichokiwasilisha Mpoki si maombi ya waleta maombi, bali ni maombi ya wakili mwenyewe.

Alidai Mpoki ameshindwa kueleza mahakama ni madhara gani ambayo wateja wao watapata ambayo hayawezi kurekebishika na hayapo katika kiapo chao, wao walichowasilisha ni tangazo la TAMISEMI.

"Kama itatokea mahakama hii ikatoa amri hii ya kuzuia, wao watapata hasara gani? Jibu ni kwamba wao hawatapata hasara wala kupoteza chochote, lakini wizara ndiyo itakayopata hasara," alidai Sanga.

Naye Wakili Erigi Rumisha alidai waleta maombi wanadai waziri hana mamlaka ya kutunga kanuni; mamlaka hayo ni ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, lakini wameshindwa kueleza ni kifungu gani cha sheria kinaeleza hayo.

Wakili Mkuu wa Serikali kutoka ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Marck Mulwambo alidai kuna utaratibu mbadala wa kufungua shauri hilo, halikupaswa kuja kwa njia ya mapitio; akaomba mahakama ikubaliane na hoja zao kwamba viapo vya waleta maombi vimekosewa.

Kesi imeahirishwa hadi Septemba 9 mwaka huu (Jumatatu) saa sita mchana kwa ajili ya kutoa uamuzi kuhusu hoja zote. Kesi hiyo imefunguliwa dhidi ya TAMISEMI na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

# Muswada Sheria Hadhi Maalum Diaspora waondolewa bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAREKEBISHO ya Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54, kuhusu hadhi maalum kwa raia wa nchi nyingine yameondolewa na serikali bungeni ili kuipa nafasi kuendelea kufanyia kazi zaidi hoja hiyo.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, akiwasilisha bungeni jana maelezo ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2024, alisema sheria hiyo ilitungwa mwaka 1995 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara 12.

Alisema serikali ilipendekeza kurekebisha sheria hiyo kwa ajili ya kuweka masharti yanayohusu hadhi maalum kwa raia wa nchi nyingine mwenye asili ya Tanzania.

"Hata hivyo, kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya serikali, baada ya mashauriano na kamati, serikali inapendekeza kuondoa marekebisho hayo yanayohusu hadhi maalum kwa raia wa nchi nyingine ili yaendelee kufanyiwa kazi zaidi," alisema.

Alieleza kuwa kifungu cha 32 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuainisha muda wa ukomo wa juu wa kutumika kwa kibali cha makazi kuwa miaka miwili na kibali hicho kinaweza kuhuishwa kwa kipindi kirefu zaidi ya miaka miwili.

"Kwa sasa, kifungu cha 32 kimeainisha kwamba muda wa ukomo wa juu wa kibali cha ukaazi kuwa ni miaka mitatu na muda wa ukomo wa juu kuhusiana na uhuishaji kibali hicho kuwa ni miaka miwili.

"Kifungu hicho pia kinaainisha kwamba muda wa jumla wa uhalali wa kibali cha ukaazi cha msingi na muda wa uhuishaji wake hautazidi miaka mitano," alisema.

Alibainisha kuwa lengo la marekebisho hayo ni kuondoa ukomo wa miaka mitano wa kibali cha ukaazi cha msingi na uhuishaji wake kwa ajili ya kuwezesha wageni kukaa na kufanya shughuli zao ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda mrefu kulingana na shughuli wanazofanya, ikiwa ni pamoja na uwekezaji.

Mwanasheria Mkuu alisema sehemu ya tatu ya muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, iliyotungwa mwaka 1985 na mpaka sasa imeshafanyiwa marekebisho mara 35, wakilenga kuleta ufanisi katika uandaaji ripoti ya uchunguzi wa kiforensiki.

"Inapendekezwa kuongezwa kwa kuainisha namna na muundo wa kuandaa ripoti ya uchunguzi wa kiforensiki kwa njia ya mtandao.

"Lengo la marekebisho haya ni kuboresha mfumo wa uandaaji ripoti ya uchunguzi wa kiforensiki pamoja na kuongeza thamani ya ushahidi wa ripoti hiyo," alisema.

Pia alisema muswada unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Serikali Mtandao, Sura ya 273 ya Mwaka 2019 ili kuweka uwiano wa adhabu na kosa lililotendeka na kuzuia watu kutenda au kujaribu kutenda kosa husika.

"Kifungu cha 57 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu kwa kosa la kuondoa, kuharibu au kubadili data, kumbukumbu za kielektroniki, mifumo au vifaa vya kielektroniki.

"Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha adhabu zinazowekwa kwenye sheria zinawekwa kwa kuzingatia uzito wa makosa," alisema.

HABARI KITAIFA

## Waziri aagiza mabasi 670 ya mwendokasi Mbagala, Kimara

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ameagiza Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), kupata mabasi 500 ya njia ya mwendo wa haraka Mbagala ifikapo Desemba.

Alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizindua rasmi kadi janja na mageti janja ambayo yatafungwa kwenye vituo vyote vya mwendokasi hali itakayowawezesha abiria kuachana na tiketi za makaratasi.

"Udart na DART shirikianeni kuhakikisha njia ya Mbagala inakuwa na mabasi 500 mpaka Desemba na kwa sababu njia imeshakamilika sitaki tena kusikia maneno ya michakato, nadhani mnanijua mimi sio mtu wa maneno maneno nataka vitendo zaidi," alisema Mchengerwa.

Alisema hata njia ya Kimara-Posta inapaswa kuongezewa mabasi hadi kufikia 170 kwa kuwa mabasi yaliyopo sasa hayatoshi na abiria wanalalamika kuchelewa vituoni kwa muda mrefu.

Aidha, alisema kama UDART na DART hawawezi kuleta mabasi hayo, basi washirikishe sekta binafsi ambayo alisema ina uwezo wa kuleta mabasi mengi.

"Msifikiri wazungu tu ndio wanaweza kuwekeza kuna Watanzania wengi tu wanaweza kuleta mabasi na tukaondokana na tatizo hili la uhaba wa mabasi, malalamiko ya mradi huu yamekuwa mengi na sitaki tena kusikia malalamiko nadhani mnanielewa," alionya.

"Watendaji DART na UDART acheni kawaida ya kujifungia ofisini tokeni nje mkaangalie huduma zinavyotolewa. Kama kuna mzembe anakwamisha huduma ondoa weka mwingine hakuna kubembelezana sisi tunataka kazi tu," alisema.

Alisema kumekuwa na malalamiko mengi ya mabasi kuwaacha abiria vituoni kwa kisingizio cha kwenda na muda hivyo aliwataka viongozi kuhakikisha wanamaliza kero hizo kwa kuwasimamia madereva wao.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi ya Yaendayo Haraka (DART), Dk. Athuman Kihamia, alisema matumizi ya kadi pamoja na mageti janja yatasaidia abiria na katika utunzaji wa mazingira na kupunguza foleni.

"Mfumo huu uliojengwa na wataalamu wa DART una faida nyingi ikiwamo kuondoa uchafuzi wa mazingira, zitasaidia kuondoa usumbufu wa chenji pia kuondoa foleni za kununua tiketi," alisema Dk. Kihamia.

Aidha, alisema kadi hizo zina ubora kulinganisha na zingine zinazotumika kwenye mataifa mbalimbali.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya DART, Dk. Florence Turuka, alisema ni jambo la fahari kuona mifumo inaimarika kwenye kuendesha usafiri wa mabasi yaendayo haraka na dhamira yao ni kuona kuwa mifumo hiyo inarahisisha na kuleta tija jijini Da es Salaam.

# Kibano wafanyabiashara wasioweka bei bidhaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imependekeza wauzaji wa bidhaa au huduma wasioonesha bei kutozwa faini isiyopungua Sh.10,000 na isiyozidi Sh. milioni moja ili kulinda watumiaji kutozwa zaidi.

Akiwasilisha bungeni jana maelezo ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, alisema marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kutatua changamoto mbalimbali zilizobainika katika utekelezaji wa masharti ya Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2023.

Alisema kifungu cha 17 pamoja na jedwali la marekebisho, kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kwa kuweka sharti la wauzaji wa bidhaa au huduma kuonesha bei ya kila bidhaa au huduma.

"Pia kifungu hiki kinaweka masharti yanayowazuia wauzaji wa bidhaa au huduma kutoza wateja bei zaidi ya ile iliyobainishwa kuwa ndiyo halisi kwa bidhaa au huduma. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kulinda walaji (watumiaji) dhidi ya kutozwa zaidi na kuhakikisha uhakika wa bei ya bidhaa au huduma kabla ya kununua," alisema.

Pia alisema kifungu cha 60 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha adhabu za jumla zitakazotumika katika sehemu ya VI na VII ya sheria.

Kadhalika, alisema marekebisho hayo ya sheria yanaipa tume mamlaka ya kipekee ya kushughulikia masuala ya kumlinda mtumiaji ili kuhakikisha watu wanaotenda makosa yanayohusu ushindani hawakwepi adhabu kwa kisingizio cha kuwa hakuwa na nia ovu wakati makosa ya ushindani ni dhahiri kulikuwa na nia pia yanakuwa au yanaelekea kuharibu soko.

Aidha, alisema vifungu vya 5 na 8 vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuanzisha dhana ya 'Hodhi ya Pamoja' na kuongeza kiwango cha hodhi ya soko kutoka asilimia 35 hadi 40 ili kuweka vikwazo dhidi ya matumizi mabaya ya hodhi ya soko inayohusisha mtu zaidi ya mmoja na kuendana na mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo yanayofanyika katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

"Vifungu vya 61 na 84 vinapendekezwa kurekebishwa ili mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Baraza la Ushindani aweze kukata rufaa Mahakama Kuu ambayo itasikilizwa na majaji watatu. Lengo la marekebisho haya ni kutoa fursa kwa mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya baraza kuweza kutafuta haki kwenye chombo cha juu zaidi cha utoaji haki,"valisema.

**MAONI YA KAMATI**

Akisoma maoni ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mwenyekiti Deodatus Mwanyika, alisema kifungu cha 17 cha sheria kimeweka masharti ya wauzaji wa bidhaa na huduma kuonesha bei za bidhaa na huduma (price indication or display) badala ya bei husika kutamkwa na muuzaji.

"Ilielezwa kosa la kukiuka masharti hayo kwa watu wa kawaida ni kutozwa faini isiyopungua sh. 300,000 na isiyozidi sh. milioni moja.

"Mheshimiwa Spika, Kamati katika uchambuzi wake ilipata wasiwasi kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki hasa kwa wajasiriamali wadogo ikiwemo wauzaji wa chakula katika maeneo yasiyo rasmi maarufu mama lishe, watembeza bidhaa maarufu machinga, bodaboda na wauzaji wa bidhaa ndogondogo magengeni.

"Wasiwasi zaidi ulionekana kwenye faini inayopendekezwa kwa kuona inaweza kuwaondoa sokoni wafanyabiashara wadogo badala ya kuwalinda na kuwakuza," alisema.

Alibainisha kuwa kamati ilishauri kwamba kwa wauzaji wa bidhaa au huduma wenye mtaji usiozidi sh.milioni nne, adhabu yao kwa kosa la kutokuonyesha bei ya bidhaa au huduma iwe ni faini isiyozidi Sh. 50,000.

"Serikali ilikubali ushauri huo kwa kuahidi kufanya marekebisho kupitia jedwali na kuweka kiwango cha adhabu kuwa faini isiyopungua Sh. 10, 000 na isiyozidi sh. milioni Moja,"alisema.

Alisema kamati imeishauri serikali kuwa tume yenyewe ndio ihusike katika usimamizi wa kifungu hiko kutokana na kuwa na utalaamu wa kipekee katika masuala ya ushindani na Wizara itunge kanuni au mwongozo kuhusu utekelezaji wake ili kuepusha matumizi mabaya ya mamlaka yanayoweza kutendeka na baadhi ya watumishi wasio waaminifu kwa kuwatoza wafanyabiashara wadogo faini kubwa kinyume na ushauri wa Kamati.

"Mheshimiwa Spika, Kuhusu kuwepo kwa masharti yanayoweka sharti la kuonyesha bei ya bidhaa na huduma, Kamati ilielezwa kuwa madhara ya kutokuonyesha bei ya bidhaa ni makubwa kwa walaji ukiwianisha na manufaa ya kuonyesha bei yake. Kwa msingi huo, ni vyema kuanza kuliko kuacha hali kama ilivyo sasa. Ni rai ya Kamati kuwa elimu ya kutosha itatolewa kabla ya kuanza kutekelezwa kwa kifungu hiki,"alisema.

Alisisitiza Kwa kuwa wauzaji wa bidhaa na huduma watalazimika kuanza kuonyesha bei ya bidhaa na huduma, Serikali itoe elimu juu jambo hili kupitia vyombo vya Habari, mitandao ya kijamii, vikao vya wadau ikiwemo vyama vya walaji na wafanyabiashara ili jambo hilo liweze kueleweka kwa jamii ya wauzaji na wanunuzi na hivyo kurahisisha utekelezaji wake.




EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: OFFICE ADMINISTRATOR** **Job Type:** Full Time

**Reports to:** General Service Officer **Location:** Tanga, Tanzania

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

**To be responsible for:**

- Ensuring the smooth running of EACOP Tanzania – Tanga Branch Office.

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

- Handle Telephone and Correspondence Management: Efficiently manage incoming phone calls, emails, letters, and packages, ensuring timely and accurate responses.
- Guest Reception and Hospitality: Greet and welcome guests upon arrival, providing a courteous and professional first impression of the office.
- Reception Area Maintenance: Maintain a clean, organized, and presentable reception area, ensuring that all necessary stationery and materials are readily available.
- Office Safety and Operations: Ensure a safe working environment for staff and visitors and oversee responsible operations of the office facilities.
- Office Supplies Management: Order and manage office supplies, including stationery, consumables, and furniture, and maintain accurate inventory records.
- Travel and Accommodation Coordination: Arrange travel and accommodation for both visiting and resident employees, ensuring logistical needs are met efficiently.
- Expense Tracking and Record-Keeping: Maintain up-to-date records of office expenses, including LUKU bills, meals, and other costs, ensuring accurate financial tracking.
- Meeting and Event Organization: Organize meetings, schedule appointments, and coordinate catering for company events, ensuring all logistical details are handled effectively.
- Additional Duties: Perform any other related tasks as assigned to support the smooth operation of the office.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

EACOP is committed to ensuring that the health, safety and welfare of workers, communities, and the environment are well addressed and managed. Therefore, the employee is mandated to:

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- Bachelor's degree in administration or any related field.
- English proficiency.

**Experience Required:**

- Minimum 4 years' experience in in a related Administration role.
- Proven ability to multitask, work independently, and manage significant workload and competing demands.
- Capable of working with minimum supervision.
- Strong interpersonal skills are required.
- Good organization skills and aptitude to work under stress.
- Good HSE (Health, Safety and Environment) knowledge and awareness.
- Competent Computer skills I.e., Word, Excel and PowerPoint.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 30th September 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

# Wapigakura wapya 491,050 kuandikishwa mikoa mitatu

**Na Mwandishi Wetu**

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imesema kuwa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mkoani Mara, Simiyu na baadhi ya halmashauri za Mkoa wa Manyara utafanyika kwa siku saba kuanzia leo hadi Septemba 10, mwaka huu na jumla ya wapiga kura wapya 491,050 wanatarajiwa kuandikishwa.

Kwa mujibu wa makadirio yaliyofanywa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na ambayo yanatokana na takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, idadi ya wapiga kura 3,391,017 wanatarajiwa kuwamo kwenye daftari hilo kwenye mikoa hiyo wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Kailima Ramadhan idadi hiyo inaweza kuongezeka zaidi.

"Idadi hii inaweza kuongezeka kwa kuwa inawezekana wapo Watanzania ambao walikuwa na sifa za kuandikishwa kuwa wapiga kura wakati wa uboreshaji wa daftari mwaka 2019/20, lakini kwa sababu moja au nyingine hawakuweza kujiandikisha kuwa wapiga kura," alisema Kailima.

Kwenye uboreshaji huo wa daftari jumla ya vituo 4,373 vitatumika kuwaandikisha wapiga kura wapya na kuboresha taarifa za wapiga kura waliondikishwa kwa miaka iliyopita.

Uboreshaji wa daftari kwenye mikoa hiyo unafanyika ikiwa ni mwendelezo wa uandikishaji uliozinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mkoani Kigoma Julai 20, mwaka huu ikiwa ni mzunguko wa kwanza uliojumuisha mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora.

Baada ya uboreshaji kukamilika kwenye mikoa hiyo ulifuata mzunguko wa pili kwenye mikoa ya Kagera na Geita na wa tatu kwenye mikoa ya Mwanza na Shinyanga.

Mzunguko wa nne wa uboreshaji wa daftari unajumuisha Mkoa wa Mara, baadhi ya halmashauri za Mkoa wa Manyara ambazo ni Halmashauri ya Mji wa Babati na Halmashauri za wilaya za Babati, Hanang na Mbulu na Mkoa wa Simiyu ambao vituo vitakuwa vinafunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni.

# Ndugulile kuanza kazi WHO Machi

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MBUNGE wa Kigamboni (CCM), Dk. Faustine Ndugulile, ameweka wazi kuwa anatarajia kuanza kutekeleza majukumu yake mapya ya Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika mwishoni mwa Machi, mwakani huku akitaja maeneo manne atakayotilia mkazo.

Aidha, Bunge limempongeza kwa ushindi alioupata kwa kuwa umeendelea kuipa Bunge na Tanzania sifa.

Akitoa shukrani kwa Bunge kwa kufanikisha kushinda nafasi hiyo, Dk. Ndugulile alisema: "Kuna swali kwamba lini nitaanza kazi, utaratibu wa taasisi hii ya kimataifa toka uchaguzi hadi unaanza kazi unapewa miezi sita, hivyo natarajia kuanza mwishoni mwa Februari au Machi 2025."

Alibainisha Jimbo la Kigamboni haliko wazi kwa sasa na yeye ndiye mbunge na bado yupo kuwaongoza wana Kigamboni.

"Bara la Afrika lina mafanikio makubwa katika sekta ya afya na changamoto na tumebakisha miaka sita kuelekea mwisho wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) na katika hili tunahitaji kuwa na mwongozo wenye maono utakaohakikisha Bara la Afrika linafanikiwa," alisema.

Alisema katika kampeni yake alisema Bara la Afrika linahitaji mtu mwenye uwezo katika masuala ya kitaaluma, kiuongozi na kisiasa ambao utamweka mwananchi wa kawaida wa Afrika kama kiungo kikuu katika utoaji huduma za afya."Nilishindana na watu ambao ni wabobezi katika taasisi hii ya WHO lakini nashukuru mawaziri wa afya walituelewa kwamba aina gani ya uongozi tunahitaji katika bara letu," alisema.

Alifafanua kuwa maeneo manne ambayo waliyazungumzia ni kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa wananchi wa Afrika, kujiandaa vizuri katika majanga makubwa yanayojitokeza kama vile corona.

"Tunakwenda kuimarisha ushirikiano na taasisi mbalimbali katika bara hili na kwa njia ya kipekee. Nilikuwa nanong'ona na Mheshimiwa Spika, wabunge tumekuwa tukiyaacha mbali katika uongozi wangu Mabunge ya Afrika yatakuwa sehemu ya kazi nitakazokuwa nazifanya nikiwa kiongozi,"alisema.

Alisema anakwenda kuiboresha WHO ili kuhakikisha inakuwa imara na kusimamia sekta ya afya Bara la Afrika na nchi zinufaike.

"Kwa sasa naendelea kujipanga nimepewa miezi sita ya kujipanga kuiangalia taasisi namna inavyofanya kazi, kuandaa maono yangu na kuhakikisha tutakapoanza kazi mwezi Machi mwakani basi tunakwenda vizuri," alisema.

"Nia ya kufanya hiyo kazi anayo na sababu ya kufanya hivyo na uwezo anao niwaombe wabunge kuelekeza sala na dua kwangu jukumu hili ni kubwa sana limebeba maono yetu na ya wana Afrika wanategemea makubwa sana," alisema.

Aliishukuru serikali ya Tanzania, wabunge na watu wote waliomuunga mkono kuwania nafasi hiyo na kusisitiza kuwa atakuwapo kwa kipindi cha mpito kupokea maoni na ushauri.

"Nafasi hii si ya kwangu ni ya Watanzania na Bara zima la Afrika, mimi ni Mtanzania wa kwanza kushika nafasi hii na mwana Afrika Mashariki wa kwanza kushika nafasi hii nakwenda kuwa kiongozi mkuu wa sekta ya afya katika nchi 47 za Bara la Afrika," alisema.

Alisema katika nafasi hiyo anakwenda kuhudumia Waafrika bilioni 1.5 na ni ya miaka mitano na endapo atafanya vizuri atachaguliwa tena kwa muda wa miaka mitano.

Katika hatua nyingine, Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu, akisoma taarifa ya Spika, alisema Bunge linampongeza kwa kushika nafasi hiyo na kwamba ameleta heshima kubwa kwa nchi.

**HABARI KITAIFA**

## FCC yataja mbinu tano kukabili uingizaji bidhaa bandia nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa mikakati mitano ya serikali kupitia Tume ya Ushindani (FCC) kukabiliana na uingizaji bidhaa bandia.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alitaja mikakati hiyo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Tarime Mjini (CCM), Michael Kembaki.

Mbunge Kembaki alihoji mkakati wa serikali kuzuia uingizaji bidhaa bandia kutoka nje ya nchi ambazo ni hatari kwa watumiaji.

Naibu Waziri Kigahe alitaja mikakati hiyo, kuwa ni kuimarisha ukaguzi katika bandari na mipaka, ikiwa ni pamoja na ufunguaji ofisi mpya katika Kanda ya Magharibi (Kigoma) na Kanda ya Kusini (Mtwara).

Alitaja mikakati yao mingine ni kuimarisha shughuli za ufuatiliaji katika soko na utoaji elimu kwa wadau ili kutambua na kuondoa bidhaa bandia sokoni.

"Pia, tunashughulikia malalamiko ya kuwapo bidhaa bandia sokoni kwa kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika maeneo na maduka yanayodhaniwa kuwa na bidhaa bandia," alisema.

Naibu Waziri huyo, alisema wameimarisha ushirikiano na wadau wa biashara, ikiwa ni pamoja na Jumuiya za Wafanyabiashara hususani katika Soko la Kariakoo, wasambazaji na wauzaji ili kuunda umoja dhidi ya bidhaa bandia.

Pia, alisema wanaimarisha mfumo wa kisheria unaohusiana na hatua za kudhibiti bidhaa bandia ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya sheria iliyopo.

Naibu Waziri huyo alisisitiza serikali kuendelea kusimamia uzalishaji na uingizaji bidhaa kwa kuzingatia ubora, usahihi wa alama na mahitaji ya nchi ili kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi na jamii.

UTUMBO NJE

# Kila wiki Muhimbili yapokea watoto saba

**Na Gwamaka Alipipi**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) inapokea wastani wa watoto watano hadi saba kila wiki wenye tatizo la utumbo kuwa nje pamoja na changamoto katika njia ya haja kubwa.

Vilevile, takwimu kutoka hospitali hiyo ya hadhi ya juu zaidi kitaifa, zinaonesha kila wiki kuna wastani wa watoto wanane wanaozaliwa na matatizo hayo.

Daktari Bingwa wa Upasuaji kwa Watoto MNH, Dk. Monica George alieleza hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kusaidia watoto wenye changamoto za afya, hususani wanaozaliwa utumbo ukiwa nje na wenye changamoto katika njia ya haja kubwa.

Kampeni hiyo imepewa jina la 'Mtoto Day Out', lengo likiwa kukusanya Sh. milioni 200 kwa ajili ya kusaidia watoto hao.

Dk. Monica ambaye pia ni Mkuu wa Idara ya Watoto MNH alisema mtoto kuzaliwa utumbo kuwa nje pamoja na kutokuwa na njia ya haja kubwa ni tatizo kubwa.

"Mtoto anazaliwa utumbo ukiwa nje, kwenye kitovu kunakuwa na tundu, utumbo badala ya kuwa ndani unakuwa nje. Pia mtoto anazaliwa bila ya kuwa njia ya haja kubwa. Ndiyo maana tunafanyia upasuaji. Haya matatizo yanaweza kubainika mapema endapo mama akifanyiwa uchunguzi wakati wa kliniki," alisema.

Bingwa huyo alisema kuwa miaka mitano iliyopita, watoto wenye matatizo hayo walikuwa wanafariki dunia kutokana na kutokuwa na utaalamu, lakini hivi sasa kuna utaalamu na wamefanikiwa kudhibiti vifo.

"Tunaomba jamii iunge mkono kampeni hii ili kupunguza vifo vya watoto wachanga. Pia wajawazito waende kliniki mapema ili kujua tatizo," alisema.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Watoto MNH, Dk. Zaituni Bokhary alisema: "Hili tatizo ni kubwa sana. Miaka ya nyuma watoto walikuwa wanakufa sana. Nchi zingine vifo ni asilimia nne lakini kwetu ilikuwa ni asilimia 100."

Alisema hali hiyo iliwalazimu kuanza kufanya utafiti ili kubaini tatizo na kugundua Tanzania inatumia njia mbadala kutibu tatizo kulinganisha na nchi zingine.

"Baada ya utafiti, tukaanza kufanya njia za kisasa na tukaanza kupata matokeo chanya na kupunguza vifo vya watoto. Kila kesi ya mtoto mwenye matatizo hayo akawa analetwa MNH moja kwa moja kabla ya kumpa huduma ya kwanza.

"Tukasema hapana, tukaanza kutoa elimu nchi mzima. Tukaanza na hospitali za Dar es Salaam namna na kumhudumia mtoto wa namna hiyo hadi anapoletwa MNH," alisema.

Dk. Zaituni alisema baada ya kutoa elimu, hospitali za Dar es Salam wakahamia mikoa ya Kigoma, Mtwara na Mbeya, wakifanikisha kupunguza vifo vya watoto hao.

Alisema mtoto mwenye utumbo nje, anapozaliwa wanamwekea mfuko maalum uitwao 'silo bag' ili kuhifadhi utumbo; gharama yake ni Sh. 60,000.

"Hii gharama ni kubwa sana. Kwa mtu wa kawaida hawezi kuimudu. Tunaomba Watanzania mtusaidie kununua mifuko hii badala ya kutegemea misaada kutoka Ujerumani.

"Huu mfuko tunauweka mara moja tu na kila siku daktari anakuwa na kazi ya kuurudisha utumbo taratibu katika njia yake hadi pale utakapokaa sehemu husika," alisema Dk. Zaituni.

Alisema gharama ya upasuaji kwa mtoto mmoja mwenye tatizo la utumbo kuwa nje ni Sh. 900,000.

Kuhusu mtoto mwenye changamoto kwenye njia ya haja kubwa, Dk. Zaituni alisema: "Tunawawekea njia mbadala ya kupata haja kubwa. Kwa siku mtoto mmoja anatumia mifuko mitatu hadi minne. Hii njia ni asilimia 40 ya Watanzania wanaweza kuimudu. Lakini operesheni ni zaidi ya Sh. milioni tano."

Alisema changamoto kwenye njia ya haja kubwa kwa watoto ni moja ya magonjwa 10 hatarishi kwa watoto; tatizo hili kwa sasa linatibika.

Dk. Zaituni alisema tatizo hilo lipo hasa kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa na mikoa ya mashariki mwa nchi. Kisababishi kikubwa ni uvutaji sigara, unywaji pombe na kurithi (genetic).

Mmoja wa waratibu wa kampeni hiyo, Dina Marious alisema ni miaka saba sasa tangu waanzishe kampeni hiyo, wakiandaa tamasha la watoto linalokuwa na kiingilio pamoja na michezo mbalimbali.

Dinna alisema: "Tunashirikiana na Hospitali ya Taifa Muhimbili kusaidia watoto hawa. Tunatarajia kufanya kampeni Desemba mwaka huu. Tatizo hili linatibika, lengo ni kukusanya Sh. milioni 200 ili kusaidia watoto hawa."



Mkandarasi anayejenga miundombinu ya mabasi ya mwendokasi akifunga taa za kuongozea magari katika barabara ya Kilwa, eneo la Mbagala, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Spika ataka miundombinu rafiki wenye ulemavu SGR

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Spika wa Bunge, Mussa Zungu ameelekeza serikali kuchukua hatua za haraka kuimarisha huduma kwa watu wenye mahitaji maalum kwenye stesheni za treni ya mwendokasi.

Alitoa agizo hilo jana baada ya Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Asha Abdullah Juma.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itaongeza idadi ya viti mwendo kwa ajili ya abiria wenye mahitaji maalum kwenye viwanja vya ndege na stesheni za SGR.

"Watu wenye mahitaji maalum wanapata shida sana kusafiri hasa kwenye stesheni za SGR, lini serikali itatoa mafunzo maalum kwa wahudumiaji wa watu hawa?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kihenzile, alisema tayari kuna viti mwendo vya umeme ambavyo vinasimamiwa na watoahuduma kwenye viwanja vya ndege.

Alisema kwenye SGR au viwanja vya ndege kuna watu wenye mafunzo ambao wanatoa huduma kwa watu hao, wakiwamo madaktari.

Kutokana na majibu hayo, Naibu Spika huyo alielekeza hatua za haraka zichukuliwe ili kuimarisha huduma kwenye stesheni hizo ili watu wenye mahitaji maalum waondokane na adha wanayoipata.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kushughulikia huduma za abiria wenye mahitaji maalum na wagonjwa kwenye viwanja vya ndege.

Kihenzile, akijibu swali hilo, alisema serikali imeendelea kuhakikisha inaweka miundombinu na vifaa wezeshi ili kuhakikisha huduma kwa abiria wenye mahitaji maalum na wagonjwa wanapata huduma stahiki katika viwanja vya ndege.

"Hii ni pamoja na kusanifu na kujenga majengo ya abiria sambamba na miundombinu wezeshi kama vile maliwato maalum (disabled toilet), ngazi za mjongeo (ramp), usimikaji ngazi za umeme (lift escalators) na kuhakikisha kunakuwa na vifaa maalum vya kuwahudumia abiria wenye mahitaji maalum pamoja na wagonjwa katika viwanja vya ndege kama vile viti vya magurudumu," alisema.

Kiongozi huyo pia alisema serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa watu wenye mahitaji maalum na wagonjwa katika foleni za ukaguzi wa abiria na foleni za kuingia ndani ya ndege kuufanya usafiri wa anga kuwa rafiki kwao.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu matumizi nishati safi ya kupikia muhimu kufikia malengo

**TANZANIA** imeanza kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia. Mkakati huo wa miaka 10 kuanzia mwaka 2024 hadi 2034, pamoja na mambo mengine unalenga kupunguza athari za tabianchi ambazo kwa sasa ni janga la dunia kutokana na kasi ya uharibifu wa mazingira.

Kasi hiyo inatokana na ukataji miti ovyo kwa ajili ya kuni na mkaa ambayo ni nishati inayotumika kwa wingi kwa kupikia mijini na vijijini. Hatua hiyo imesababisha mabadiliko ya tabianchi. Kwa kutambua hilo, serikali ya sasa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imechukua hatua madhubuti za kukabiliana na uharibifu wa mazingira na athari zake kiuchumi.

Hatua hiyo inaeleza kinagaubaga kwamba ongezeko la uharibifu wa mazingira lina athari kubwa kiafya, kiuchumi na kijamii hasa kutokana na mahitaji makubwa ya nishati ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia ambayo si salama.

Kutokana na ukweli huo, serikali imeanzisha mkakati huo jumuishi, ambao umeandaliwa ili kutekeleza Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 ambayo pia inaweka bayana kwamba ongezeko la matumizi ya nishati isiyo safi na teknolojia zisizo sanifu za kupikia, yamechangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira na matatizo ya kiafya kwa watumiaji.

Kwa mantiki hiyo, mkakati huo unalenga kuboreha maisha ya wananchi kupitia matumizi ya nishati za kisasa za kupikia ikiwamo matumizi ya majiko na vifaa sahihi vya kupikia ambavyo ni mbadala wa kuni na mkaa. Msisitizo mkubwa katika hilo ni matumizi ya gesi ya kupikia pamoja na majiko sanifu yanayotumia teknolojia ya kisasa.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema juzi wakati akifungua Jukwaa la 24 na Mkutano wa Kamati ya Kudumu ya Fedha ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) kuwa kupitia mkakati huo, hadi kufikia mwaka 2034 lengo ni kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati hiyo safi.

Dk. Mpango alisema Tanzania imekuwa kinara wa bara la Afrika kwa ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia nyumbani (AWCCSP) kupitia Rais Samia ambaye amekuwa bingwa wa kipaumbele katika kusimamia suala hilo. Rais Samia amekuwa mstari wa mbele katika ajenda hiyo ambayo lengo mojawapo ni kuwaondolea wanawake mzigo wa kutumia kuni na mkaa kupikia.

Kwa ujumla, lengo la kufikia asilimia 80 wakati wa kutamatika kwa mkakati huo ni zuri kwa kuwa litawezesha maisha ya Watanzania kuimarika kiuchumi na kijamii pamoja na kiafya kutokana na matumizi ya nishati safi. Ukataji ovyo wa misitu hatimaye kusababisha jangwa na kutoweka kwa baadhi ya viumbe adhimu, yatapungua.

Licha ya kuwapo kwa malengo hayo, kuna umuhimu mkubwa wa kutoa elimu kwa kiasi kikubwa kwa watu ili kutambua umuhimu wa matumizi ya nishati hiyo kwa ustawi wa maisha. Mkakati huu nimtambuka kwa maana kuwa unahusisha sekta mbalimbali, hivyo kila mdau anapaswa kushiriki kwa nafasi yake.

Pamoja na kutolewa kwa elimu kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia, suala la gharama za gesi na majiko sanifu ya nishari rafiki zinapaswa kupewa kipaumbele ili kuwezesha Watanzania wengi kutumia nishati hiyo.

Uwezo wa kiuchumi wa wananchi hasa waishio vijijini ni mdogo, jambo ambalo linaweza kuwa kikwazo kwao kununua, hivyo inaweza kuwa chanzo cha kutofikiwa kwa malengo hayo. Kutokana na ukweli huo, ni vyema serikali ikaangalia uwezekano wa kupunguza gharama ikiwamo kutoa ruzuku katika gesi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Joyce Lameck

# Vijana mkitumia ubunifu, mitandao kijamii mnatoka

**WAJASIRIAMALI** waliofanikiwa zaidi wanaooneka zama hizi wanaelezwa kuwa, walianza safari zao katika umri mdogo, wote wana njia na mbinu tofauti zilizowafikisha kwenye mafanikio wanayoyaona sasa.

Baadhi ya vijana wanaoelekea kuwa mamilionea ni pamoja na Fahad Awadh mwenye kiwanda cha kuchakata korosho Zanzibar wengine ni Idris Sultan aliyekuwa mshindi wa shindano la Big Brother Africa 2014 na pia wapo wengine kama Brigitha Faustin na Rahma Baju.

Baadhi ya vijana hawa wanaripotiwa na Jarida la Forbes la Marekani kuwa wana nafasi ya kuwa mamilionea wa Tanzania.

Vijana hao wanaonesha uwezo wa kuunda mazingira ya kibiashara kutokana na juhudi na ubunifu, yote yakijulikana nje na ndani ya nchi pia wakifanikishwa na teknolojia na mbinu za kisasa.

Wengine pamoja na kujiajiri wanawapa fursa mbalimbali vijana wenzao kwa kuwaajiri na kuleta mafanikio katika umri mdogo wa wadau wanaoshirikiana nao.

Ni wakati wa vijana kuamka maana walio wengi wamekuwa wakilalama kuhusu changamoto ya ajira na kukosa kazi na kelele za maisha magumu yanayowakabili.

Vijana ambao ni kundi kubwa, idadi yao inatajwa katika Sensa ya Watu na Makazi ya 2022 kuwa ni zaidi ya asilimia 65 wanahitaji juhudi binafsi na za wadau ili kubadilisha maisha yao kupitia biashara na uwekezaji.

Pia vijana hawa, licha ya kwamba wanataka kuwapo na mapinduzi ya mfumo wa elimu yatakayowahakikishia mitaala inayowaandaa kwa kuwapa elimu itakayowawezesha kushiriki kikamilifu na kuwa washindani kwenye soko la ajira ni jambo ambalo linawezekana lakini siyo suluhu ya kila mmoja.

Takwimu zimethibitisha hayo kwa kuainisha kuwa, idadi ya ajira zinazopatikana zimezidiwa na wingi wa vijana wanaoingia rasmi kwenye soko la kazi wanaofikisha umri wa kujiajiri au kuajiriwa pamoja na wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu.

Teknolojia ni moja ya mambo yanayoweza kuwasaidia vijana kujikwamua na kulia na kulalamikia ukosefu wa ajira, simu janja ni fursa kubwa ya kukuza biashara kwa kutumia mitandao ya kibiashara na ya kijamii kutangaza bidhaa zao kwa wateja wa nje na ndani.

Pia, kwenye mitandao ya kijamii na kibiashara, wateja wanavutiwa kwa kuona bidhaa na kupata mawasiliano kwa urahisi jambo linalohitaji pia uaminifu.

Njia hii huenda italeta unafuu na tija katika biashara zao badala ya kuzitumia simu kwenye mambo yasiyokuwa na faida, watumie simu kujijenga kimaisha ili wajikwamue kimaisha na kuondokana na umaskini.

Kupitia teknolojia kijana ataweza kulipa kodi na kujipatia kipato. Kwa mfano, kutangaza kwenye instagram atatangaza biashara kwa kuchapisha mambo mbalimbali kuanzia mavazi, mazao ya shamba, mifugo na maua ambayo yatajulikana kwa watu na kuvutia wateja mbalimbali.

Hivyo, kupitia mitandao ya kijamii na ya kibiashara anaweza kutanua wigo wa biashara na kuongeza kipato chake na kukuza uchumii wa nchi, kwa sasa ndiyo njia rahisi ya kumfanya kijana kuwa na wateja wengi na kufanya biashara kwenda kwa haraka tofauti na awali.

Vilevile, kupitia teknolojia vijana wanapata wigo mpana wa kutambulisha biashara, hususani kwa mataifa mengine kwa sababu teknolojia imewasogeza watu karibu kimawasiliano. Hivyo, hii inaonesha ni kwa kiasi gani teknolojia itafanya vijana wajasiriamali kupiga hatua ya bidhaa wanazojihusisha nazo kwani soko ni kubwa na kuwapata wateja wapya kila wakati inawezekana kupitia simu janja.

Ni wakati wa vijana kutumia fursa hii ili kukuza soko la biashara zao ambazo kwanza ni lazima wazisajili, watumie taasisi za kuhakiki ubora na usalama kama Shirika la Viwango (TBS) na Mamlaka ya Vifaa Tiba na Dawa (TMD).

Hivyo basi, vijana wajaribu kujiajiri kupitia biashara mfano, kuuza mboga zinazozalishwa kwa kilimo hai (kisicho na kemikali), kutengeneza bidhaa za kitamaduni na kiasili kutoka makabila mbalimbali kama vyombo vya kulia, mapambo ya kuchonga, kuchora na kusuka.

Kadhalika kuandaa migahawa yenye vyakula vya Kiafrika na Kitanzania halisi, badala ya kutegemea chips na mayai, pilau, chapati na biriani ambavyo si asili ya Mtanzania.

## TIRA yaombwa kufanya ukaguzi kukabili bima feki

**Na Grace Mwakalinga**

WADAU wa bima za vyombo vya moto wameomba Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye kampuni na mawakala wanaohusika na utoaji huduma hiyo ili kudhibiti wimbi la bima feki.

Sady Mwang'onda, Mkurugenzi wa SMJ Enterprises and Insurance, alisema juzi kuwa kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wateja wakidai kukata bima za vyombo vya moto, lakini wanapopata madhila hawapati huduma kama walivyoahidiwa.

Mwang'onda aliomba TIRA kuchukua hatua za kisheria dhidi ya kampuni au mawakala watakaobainika kutoa bima feki ili kudhibiti hali hiyo ambayo inasababisha watoa huduma wasiaminiwe.

Aliwaomba wateja kuwa makini wanapotafuta kampuni na mawakala wanaohusika na ukataji bima zilizohakikiwa ili kuepuka kuingia mikononi mwa watu wasio waaminifu, akiwaita "makanjanja".

"Bima ni kinga ambayo mtu analipia ili kukinga vitu vyake vya thamani kwa ajili ya kumsaidia kukabiliana na matatizo yanayojitokeza baadaye, hivyo inasaidia kumfidia mtu dhidi ya madhara yatakayotokea," alisema Sady.

Alisema kinachochangia wateja kuingia kwenye mtego wa kukatiwa bima feki ni kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu bima halali, alidai katika kampuni yake imekuwa inatoa elimu kwa wateja kuzitambua bima hizo.

Aliongeza kuwa njia ya kuzitambua bima feki ni kufanya uhakiki kwa kutumia simu ya mkononi ambapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imetoa orodha ya kampuni na mawakala wote wanaopaswa kutoa huduma.

Akizungumzia malalamiko ya fidia ndogo kwa wateja, Sady alisema kumekuwa na udanganyifu katika utoaji taarifa sahihi kuhusu gharama halisi ya chombo cha moto kilichokatiwa bima, jambo ambalo linaleta usumbufu wakati wa kuweka thamani ya gharama halisi.

Aliwaomba wateja kutoa taarifa sahihi katika kukamilisha mchakato wa bima, ili kuondoa urasimu kwa kuwa malengo ni kufidia na kurejeshea mtu hali ya awali pindi anapopata matatizo.

Kuhusu gharama kubwa ya kukata bima, alisema TIRA imeweka viwango sawa kila kampuni na kwamba wanapokea malalamiko kuhusu gharama kubwa na aliiomba mamlaka kuangalia upya suala hilo ili kupata wateja wengi.

Agosti 31 mwaka huu, akiwa visiwani Zanzibar, Kamishna wa Bima Tanzania, Dk. Baghayo Saqware wakati wa kikao na wadau wa kampuni za bima visiwani humo, alisema kampuni na mawakala wanapaswa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kukata bima ikiwamo za vyombo vya moto na bima ya maisha.

Alizitaka kampuni na mawakala kuisaidia serikali katika mapambano ya kudhibiti wimbi la bima feki, ikiwamo kutoa taarifa za siri kwa wanaohusika na kuongeza kuwa wanaendelea kufanya ukaguzi na uchunguzi kuwabaini wanaohusika na suala hilo.



Wanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Majengo, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakicheza wakati wa mahafali yao shuleni hapo, hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wafanyakazi TPA wafurahia uwekezaji wa DP World

**Na Idda Mushi,**
MOROGORO

WAFANYAKAZI wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) wamesema ujio wa mwekezaji DP World haujawaathiri katika utendaji kazi wao bali umeongeza ufanisi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Shughuli za Meli na Bandari (DOWUTA), Muharami Manyara, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa baada ya kufanyika mkutano wa 36 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi.

Alisema wafanyakazi na chama hicho wako katika hali ya amani na utulivu na kupitia Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), menejimenti na serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, wanaamini mchakato wowote utaendelea kuwa shirikishi na haki za wafanyakazi zitaendelea kulindwa na uhusiano mzuri baina ya mwajiri na mfanyakazi.

"Usimamizi wa meli na bandari ulikuwa na waajiri watatu; MCCL kwa upande wa marine ambapo changamoto zilizopo zinaendelea kutatuliwa na serikali.

"Ya pili ni TICTS, lakini sasa inaitwa Tanzania East Africa Gateway Terminal L.T.D, halikadhalika TPA ambayo ndio tumepata mabadiliko na yakasemwa mengi, lakini sasa tunashukuru tunakwenda vizuri, na tayari kampuni ya DP World imeshaanza kazi, na wafanyakazi wa TPA wamehamia DP World bila matatizo yoyote na kuna utulivu wa hali ya juu," alisema.

Muharami alisema kwa sasa wanaendelea na mazungumzo kati ya chama na mwajiri huyu mpya DP World, ili kufungua tawi jipya la chama cha wafanyakazi na makusudi yao ni kuongeza zaidi ya wanachama.

Alisema kuwa, awali baada ya ujio wa mwajiri mpya aliyeanza shughuli zake za uendeshaji bandarini Aprili 7 mwaka huu, walitoa fursa kwa wafanyakazi wanaotaka kuajiriwa na DP World kwenye mchakato huru na usio na shuruti na walioshindwa walipewa maslahi yao stahiki kwa mujibu wa mkataba wa ajira.

"Inawezekana kwenye kazi zetu tunaweza kukutana na changamoto,vikwazo na vitu vingine, lakini kwa sasa niwe muwazi, tunakwenda vizuri kichama, kitaasisi na katika uongozi wetu," alisisitiza Muharami.


Mwenyekiti wa DOWUTA Bandari ya Dar es Salaam, Mashaka Karume, alisema utulivu uliopo kwa sasa bandarini hapo umechangiwa na elimu iliyokuwa ikitolewa kwa wafanyakazi kuhusu mabadiliko yaliyofanyika.

"Kwa kituo cha Dar es Salaam hadi sasa hali ni shwari, ikumbukwe tangu Januari, mwaka huu hadi sasa tulikuwa na pilika za ubinafsishaji kati ya DP World na TPA," alisema.

"Lakini tunamshukuru Mungu menejimenti na chama cha wafanyakazi tulifanya jitihada za makusudi kuhakikisha hali ya utulivu inakuwapo kiwandani na hadi sasa hali bado ni tulivu," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Watumishi 219,000 kupanda vyeo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 252.7 kwa ajili ya kupandisha vyeo watumishi wa umma 219,924 mwaka huu wa fedha.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Deus Sangu, aliyasema hayo jana alipojibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Janejelly Ntate.

Mbunge huyo alitaka hatua serikalini dhidi ya alichokiita "Watumishi kurundikana kwenye cheo kimoja kwa kukutana wote wa miaka mitatu hadi minne".

Alihoji, "Hamwoni kwamba hali hii itakuwa imeathiri mtiririko wa kupanda vyeo?"

Naibu Waziri Sangu alijibu kuwa serikali inatambua waliosahaulika katika uhakiki wa vyeti feki na kumtoa hofu mbunge kuwa kwa mwaka 2024/25 watazingatiwa.

"Bajeti imezingatia haya yote aliyoyasema mbunge ili kuweka msawazo kwenye upandishaji huo," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kuwasaidia walioguswa na mwongozo wa waraka wa miaka minne baada ya serikali kurejea kwa upandaji madaraja kwa miaka mitatu.

Naibu Waziri Sangu alijibu kuwa kwa mujibu wa miundo ya maendeleo ya utumishi wa kada mbalimbali na miongozo mingine, muda wa watumishi kutumikia cheo kimoja kabla ya kupandishwa kwa watumishi walioajiriwa kwa mara ya kwanza katika utumishi wa umma ni angalau kipindi cha miaka mitatu.

Alisema katika kipindi cha uhakiki wa vyeti na watumishi hewa, baadhi ya watumishi walichelewa kupandishwa vyeo.

"Katika kukabiliana na changamoto hiyo, serikali imechukua jitihada mbalimbali za kuoanisha na kuwianisha upandaji vyeo wa watumishi ambapo katika mwaka wa fedha 2022/23 imepandisha watumishi 180,000 wakiwamo walioathirika na zoezi hilo," alisema.

Naibu Waziri Sangu alisema kuwa katika utekelezaji ikama na bajeti ya mwaka 2023/24, serikali imewapandisha vyeo watumishi zaidi ya 216,000, wakiwamo walioathirika na uhakiki wa vyeti na watumishi hewa.

Baada ya kuingia madarakani, Rais John Magufuli alitangaza kufanya uhakiki wa watumishi hewa na wenye vyeti feki, hatua iliyosababisha serikali kutoajiri watumishi wapya na kutowapandisha vyeo walioukuwapo kwa takriban miaka mitatu.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua kadi janja kwa wasafiri wa mabasi yaendayo haraka, Kimara mwisho jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Afa maji kwa kutumbukia mtoni

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Somangamtama, Kata ya Njianne, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, Zuweha Akili (14), amefariki dunia baada ya kuzama Mto Mikeleng'ende alikokwenda na wenzake kufua nguo.

Viongozi wa kijiji hicho wamethibitisha kutokea kwa kifo hicho Agosti 27, mwaka huu.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Njianne, Zanifa Rwambo, alisema kuwa siku ya tukio Zuweha, akiwa na wenzake watatu, saa tisa alasiri, walikwenda kwenye mto huo kufua.

Alisema kuwa, baada ya kumaliza kufua aliamua kuoga mtoni, wakati anajiandaa kuingia mtoni, ghafla aliteleza na kuzama ndani ya kina kirefu cha maji.

Rwambo alisema wenzake baada ya kumwona mwenzao akitapatapa walijaribu kumwokoa bila mafanikio, ndipo waliamua kuomba msaada kutoka kwa wananchi walioukuwapo karibu na eneo la mto huo.

Alisema walipofika eneo hilo, walimtafuta msichana huyo bila mafanikio na kuamua kutoa taarifa kwa uongozi wa kijiji na kata kuendelea na kazi ya kumtafuta na kufanikiwa kuupata mwili wake siku ya pili saa 10 alasiri.

"Baada ya kuona jitihada zao zinagonga mwamba, waliomba msaada kwa watu waliokuwapo eneo lile wasaidie kumwokoa mwenzao," alisema Rwambo.

Diwani wa Njianne, Rajabu Ngatanda, alithibitisha kutokea kwa kifo cha binti huyo na kuwataka wananchi wa kata hiyo kuchukua tahadhari wanapokwenda maeneo ya mito ili kulinda usalama wao.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, John Imori, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo huku akiwataka wananchi kuchukua tahadhari na kutoruhusu watoto kwenda mtoni peke yao.

# Mawasiliano miongoni mwa mashine yazidi kuimarika

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema mawasiliano baina ya vifaa vinavyojiendesha vyenyewe bila ushiriki wa binadamu yanakua nchini.

Uongozi wa mamlaka hiyo umesema laini za simu kwa matumizi ya mashine kwa mashine zimeongezeka kwa asilimia 4.3 ndani ya miezi mitatu.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Ubora wa Huduma za Mawasiliano, kuna laini 962,928 zilizotumiwa na mashine Juni 2024 kulinganisha na laini 937,257 Aprili mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema katika laini hizo Vodacom inaongoza kwa laini 551,541 ambazo ni asilimia 57.3 ya laini zote, ikifuatwa na Airtel yenye 329,292 (asilimia 34.2) na Halotel ikiwa na laini 57,340 (asilimia 6.0) na Tigo 24,755.

Alisema TTCL haina laini za mashine kwa mashine (M2M) na kwamba imepoteza laini 299 zilizokuwa zimesajiliwa Aprili 2024.

"Teknolojia ya mawasiliano baina ya mashine bila kuingiliwa na binadamu inayojulikana kwa kifupisho cha lugha ya Kiingereza "M2M", inawezesha vifaa kuwasiliana yenyewe na kubadilishana data na taarifa bila ushiriki wa binadamu," alisema.

Dk. Bakari alitaja mifano ya teknolojia hiyo ni mita za kisasa za umeme na matumizi ya nishati, kamera za usalama wa maeneo ambavyo vinaweza kutuma taarifa kwenye simu ya mkononi ya mmiliki akiwa mbali.

"Hii inamwezesha kufuatilia matumizi na matukio muda wote akiwa mbali. Matumizi mengine ni kwenye mifumo ya usambazaji bidhaa ambapo majokofu ya kisasa yanaweza kuagiza vitu kwenye maduka kadri vinavyopungua," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Bakari, teknolojia pia inatumiwa kwenye vifaa vinavyovaliwa na wahusika, mithili ya saa za mkononi ili kufuatilia afya, ukakamavu na shughuli za kila siku za mhusika.

"Vinahamisha taarifa kwenye vyombo vingine kama vile simu janja na kompyuta zilizounganishwa kwenye mitandao," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema vifaa vya kuvaa mwilini 7,721 vilikuwa vinatumika Tanzania Juni 2024, na kwamba kwa ujumla, laini za simu kwa mawasiliano baina ya watu na za M2M ziliongezeka kutoka 73,553,890 Aprili hadi 76,550,934 Juni 2024.

Alisema mwenendo wa usajili wa laini za aina zote kati ya 2019 na Juni mwaka huu unaonesha ongezeko la asilimia 60.53 kutoka laini 47,685,232 hadi 76,550,934.

"Takwimu hizo pia zinaonesha kuwa gharama za vifurushi au bando kwa data zimeshuka kwa asilimia 0.6 kati ya Aprili na Juni," alisema Dk. Bakari.

Alieleza kuwa wastani wa gharama za maongezi kwenye mtandao wa mtumiaji na kwenda mitandao mingine zilianza kukaribiana mwaka 2020 kufuatia kushuka kidogo kidogo miaka iliyotangulia.

Alisema gharama za maongezi kwenye mtandao wa mtumiaji zilishuka kutoka Sh. 149 kwa dakika mwaka 2019 hadi Sh. 26 mwezi Juni 2024, huku gharama kwenda mitandao mingine zilishuka kutoka Sh. 189 kwa dakika hadi Sh. 28.

Alisema kiwango cha kila mwaka cha ukuaji wa simu za maongezi kwenda mitandao mingine kilikuwa mara saba ya kile cha simu ndani ya mtandao wa mtumiaji kati mwaka 2019 na 2023.

"Wakati simu ndani ya mtandao ziliongezeka kwa asilimia tisa kwa mwaka kipindi hicho, simu za watumiaji kwenda mitandao mingine zilipaa kwa asilimia 61. Dakika za simu kwenye mtandao wa mtumiaji zimeongezeka kutoka 55,812,036,633 mwaka 2019 hadi 77,770,241,513 mwaka 2023. Dakika kwenda mitandao mingine zimeongezeka kutoka 11,570,993,820 hadi 67,100,445,506," alisema.

Alisema kushuka kwa gharama za simu kwenda mitandao mingine kumechangiwa na kupunguzwa kwa gharama za kuunganisha simu baina ya mitandao.

"Gharama za kuunganisha zimeshuka kutoka Sh. 15.6 Januari 2018 hadi 1.76 Januari 2024," alifafanua.



## Walimu wastaafu waomba ushirikishwaji katika miradi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WALIMU wastaafu zaidi ya 500 kutoka Mji wa Moshi mkoani Kilimanjaro na Lushoto Mkoa wa Tanga wameiomba serikali kuwatumia katika uwekezaji wa miradi ya maendeleo.

Walisema hayo juzi katika mkutano wao wa pamoja uliofanyika katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Baadhi ya walimu hao akiwamo Kasimu Sindaso, aliiomba serikali kuwatumia wastaafu katika uwekezaji.

"Serikali inapaswa kutambua kuwa kustaafu siyo kama unasubiri kufa, kustaafu ni sehemu ya kubadilisha kazi, kwa sasa wapo wastafu wanamiliki miradi ya Sh. milioni 50 mpaka Sh.milioni 100, hivyo tunavyosema ni wawekezaji ni kwamba wanaweza kutoa ajira zaidi kwa vijana ikiwa tu kutakuwa na ushirikiano," alisema Sindaso.

Alisema wao kupitia chama chao cha akiba na kukopa kilichoko Lushoto, wamefanikisha kununua magari ya kusafirisha abiria mikoani pamoja na kukopesha watu binafsi.

January Mallya alisema ikiwa serikali itawatumia walimu wastaafu wataweza kuwekeza kwenye miradi mbalimbali na tatizo la ajira litageuka kuwa historia.

Meneja wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Walimu Mjini Moshi, Bosco Simba, alisema walimu hao ni wanachama kwa zaidi ya miaka 30.

Alisema: "Tunawapatia mafunzo na kuwapa elimu ya namna bora ya kufanya mazoezi ili kuboresha afya zao, kwa hapa tumewaletea sera bora ya uwekezaji pamoja na njia ya kupata taarifa sahihi bila kurubuniwa kwa kile walichokichumia kwa miaka yao yote".

**Alisema wao kupitia chama chao cha akiba na kukopa kilichoko Lushoto, wamefanikisha kununua magari ya kusafirisha abiria mikoani pamoja na kukopesha watu binafsi.**

# Rutazaa afichua kiini kufa vikundi vingi vya vikoba

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Jamii la Tusonge CDO, Aginatha Rutazaa, amesema vikundi vingi vya wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 vinakufa kwa sababu vinapoingia kwenye muunganiko, maslahi binafsi yanatawala zaidi na kumeza maslahi ya kikundi.

Alisema hayo jana katika Kata ya Majengo, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wakati wa kuvunja mzunguko wa 16 wa kikundi cha Amkeni Vicoba Group.

Aginatha alisema chanzo kikubwa cha kufa vikundi vingi, ni matumizi ya ovyo na wanachama kukosa nidhamu ya fedha.

"Ukichunguza matumizi ya siku ya wanachama wengi ni matumizi ya ovyo. Mgeni amekuja nyumbani kwake anakimbilia kumuuliza unakunywa soda gani, kwani mgeni kakwambia umnunulie soda?," alisema na kuongeza:

"Unaingia kwenye matumizi yasiyo sahihi, nidhamu ya fedha ni pamoja na kujizuia kufanya vitu ambavyo ukiviangalia mbele havina matokeo. Sio kukufaidisha tu wewe, matokeo ya kufaidisha pia familia yako na jamii kwa wigo wake".

Zaidi aliongeza, "Nidhamu ya fedha ni kitu muhimu na ndiyo siri ya mafanikio.

Watu waliojenga maghorofa, wenye kampuni kubwa, wenye maisha ya kufuru, ni watu walioanza na mtaji wa Sh. 10,000 hadi Sh. 20,000, wauza karanga, wapiga viatu rangi waliokuwa na nidhamu ya fedha. Leo hii wenye kampuni kubwa walioajiri watu na wanaoweza kupata kipato kikubwa ambacho kinasaidia serikali yetu na kusaidia ustawi wa Tanzania".

Mwenyekiti wa Amkeni Vicoba Group, Grace Komba, alisema kikundi hicho kilichoasisiwa na Shirika la Tusonge CDO, mpaka sasa kimefikisha mtaji wa Sh. milioni 62.5.

Kabla ya kutoa taarifa hiyo, kikundi hicho kilifanya matendo ya huruma kwa kupeleka misaada ya kibinadamu katika kituo cha kulea watoto wenye mtindio wa ubongo na wenye ulemavu wa viungo cha BCC Majengo, kinachohudumiwa na Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Aidha, Diwani wa Kata ya Majengo, Humphrey Mosha, alikipongeza kikundi hicho kwa kuwa kinara wa mafanikio ya kiuchumi kati ya vikundi vyote vya wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 vilivyoko katika Manispaa ya Moshi.




Wagonjwa wa macho wakipatiwa matibabu wakiwa kwenye kambi ya siku tatu ya matibabu bure, iliyotolewa kwa ufadhili wa Mo Dewji Foundation, katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga juzi. Wagonjwa 4,228 walionwa, kati yao 376 walifanyiwa upasuaji na 1,999 walipewa miwani bure ya kusomea. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Bilioni4/- kukamilisha ujenzi Chuo cha Uhasibu Manyara

**Na Allan Isack,** BABATI

SERIKALI kupitia Wizara ya Fedha imetoa Sh. bilioni nne kwa ajili ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Kampasi ya Babati mkoani Manyara.

Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, alisema hayo wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi awamu ya kwanza katika kampasi hiyo.

"Kwa kutambua umuhimu wa mradi huu, serikali kupitia Wizara ya Fedha iliona umuhimu wa kuongeza nguvu mlipoanza ujenzi kwa kutoa ruzuku ya Shilingi bilioni nne, ili majengo haya yakamilike kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa," alisema Nchemba.

Hivyo, aliuagiza uongozi wa IAA kuendelea kubuni mitaala itakayokuwa na manufaa kwa jamii ambayo itawawezesha wahitimu kupata elimu ya ujuzi na maarifa ya kutatua changamoto mbalimbali za jamii.

Alisema mitaala hiyo inapaswa kuwa na uwezo wa kuwaandaa wahitimu waweze kujiajiri na kuajiriwa katika sekta za umma na binafsi, waweze kuchangia maendeleo ya uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja.

Vilevile alisema ujenzi wa kampasi hiyo ni matokeo ya mahitaji ya kuongeza uwezo wa chuo hicho katika kutoa elimu bora inayokidhi soko la ajira.

Naye Mkuu wa IAA, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema mradi huo kwa awamu ya kwanza utajumuisha jengo la taaluma, mabweni na bwalo la chakula.

Alisema ujenzi wa jengo la taaluma lenye ghorofa tano limefikia asilimia 98 na litakuwa na uwezo wa kuchukuwa wanafunzi zaidi ya 2,700 kwa wakati mmoja.

Alisema jengo hilo lina vyumba vya madarasa, kumbi za mikutano, maabara za kompyuta, maktaba na ofisi za wafanyakazi.

Alisema majengo yote matatu hadi kukamilika kwake yatagharimu Sh. bilioni 10, kwamba jengo la taaluma litagharimu Shilingi bilioni tano, mabweni mawili Shilingi bilioni nne na bwalo la chakula Shilingi bilioni moja.

Kadhalika alisema wanatarajia kujenga majengo mengine makubwa mawili ikiwamo jengo la utawala na TEHAMA yatakayogharimu Sh.bilioni 8.4 na kila jengo litagharimu Sh. bilioni 4.2.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa IAA, Dk. Mwamini Tulli, alisema baraza hilo litaendelea kusimamia chuo kuhakikisha mipango hiyo inatekelezwa kwa ufanisi mkubwa na majukumu yake ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.





# Mbunge aonya kitendo wezi wa mifugo kukamatwa, kuachiwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MBUNGE wa Ushetu mkoani hapa, Emmanuel Charahani ameonya kuwa kitendo cha watuhumiwa wa wizi wa mifugo kukamatwa na kuachiwa kitasababisha wananchi kujichukulia sheria mkononi dhidi yao.

Charahani, alitoa onyo hilo juzi katika kikao cha baraza la madiwani wa Halmashauri ya Ushetu cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25.

Alisema kukithiri wizi huo kumegeuka kero kwa wananchi, hivyo kunaweza kusababisha kuanza kujichukulia sheria mkononi watakapowabaini wezi hao.

Alisema amepokea malalamiko hayo kutoka kwa wananchi wakati wa mikutano ya hadhara kuwa kimeibuka kikundi cha watu wachache kinachojihusisha na wizi huo kwenye kata zenye wafugaji.

alisisitiza kuwa, atashirikiana na wananchi kuwakamata wezi wa ng'ombe na kuchukuliwa hatua ili kukomesha vitendo hivyo.

Alilitaka Jeshi la Polisi kushirikiana na sungusungu wa kila kata kutokomeza wizi huo na kufanya mikutano kuweka mikakati ya kukomesha na sio kuwashikilia kwa kuwaachia kwa kutawavunja moyo askari hao wa jadi kufanya kazi kwa kujitolea kulinda amani.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Gagi Lala alithibitisha kukithiri kwa wizi huo na kuviomba vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana na sungusungu kudhibiti.

Akizungumzia madai hayo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi alidai hana na kuahidi kufuatilia kwa kushirikiana na maofisa wa jeshi hilo wa kila kata.

Magomi, aliwataka wananchi na sungusungu kuendelea kutoa taarifa zinazofanikisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao na kufikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake dhidi ya watakaopatikana na hatia.




Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Manyara, Wolter Kirita (kushoto), akimkabidhi Mkurugenzi wa M/s Jisham & Construction, Juma Swai, nyaraka za mikataba ya miradi ya maji kwenye baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Hanang' baada ya kutiliana saini, mjini Babati juzi. Wa pili kulia ni Mkuu wa Mkoa huo, Queen Sendiga. **PICHA: GIFT THADEY**

# Samia aahidi ushirikiano taasisi za dini

**Na Vitus Audax,** MUSOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameahidi serikali iko tayari kuendeleza ushirikiano baina yake na viongozi wa kanisa katoliki ili kufikia malengo ya kuwahudumia wananchi.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi kwa niaba yake na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi wakati alipomwakilisha katika Jubilee ya Miaka 40 ya Upadre na miaka 17 ya Uaskofu wa Askofu Michael Msoganzila wa Jimbo Katoliki la Musoma. Ndejembi, alisema Rais Samia anampongeza Askofu Msoganzila kwa kutimiza miaka 40 ya upadre na kumshukuru kwa kuitumia vizuri kuwahudumia watu, akimtanguliza Mungu katika maisha yake kuliko matamanio ya kawaida ya kibinadamu na kumfanikisha katika maisha yake.

Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mwadhama Kadinali Polycarp Pengo, alisema kupitia maadhimisho hayo wanakumbushwa kutoa shukrani kwa Mungu kwa neema maisha ya Watanzania.

"Katika Injili tunaona watu 10 waliponywa na Yesu, ni mmoja tu ndiye aliyerudi kwa Bwana kumshukuru, lakini wengine tisa hawakurudi tena kutoa shukrani zao," alisema Mwadhama Kadinali Pengo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Gerald Musabila, alisema mkoa huo unatambua na kuheshimu kazi nzuri inayofanywa na Kanisa Katoliki nchini na kuahidi wataendelea kutoa ushirikiano kwa kanisa hilo na viongozi wake wakati wote.

# MSD yaboresha huduma kwa wananchi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

KAIMU Meneja wa Bohari ya Dawa (MSD) Kanda ya Magharibi, Rashid Omari amesema wamebadili muda wa usambazaji dawa na vifaa tiba kutoka kila baada ya miezi sita hadi miezi miwili ili kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kwa wakati.

Omari alitoa kauli hiyo juzi, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu Maadhimisho ya Miaka 30 ya MSD tangu kuanzishwa kwake mwaka 1994.

Alisema kwa sasa wanasambaza dawa mara sita kwa mwaka tofauti na awali walikuwa wakisambaza mara mbili lengo likiwa ni kuimarisha upatikanaji dawa katika vituo vya afya na kuboresha miundombinu ya ufikishaji dawa hizo katika vituo vyote.

"Katika kanda yetu inayohudumia mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi tutaendelea kupeleka dawa za kutosha kwa wananchi, kila baada ya miezi miwili tunasambaza tani 40 hadi 50 wakati huko nyuma tulikuwa tunasambaza tani tano hadi 10 kila baada ya miezi sita," alisema Omari.

Meneja Mawasiliano na Uhusiano MSD, Etty Kusiluka, alisema serikali imeendelea kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kusambaza dawa katika vituo vyote 8,200 vya afya nchini.

Kusiluka, alisema MSD imejenga maghala makubwa ya kuhifadhia dawa Dodoma na Mtwara ili kurahisisha usambazaji dawa katika mikoa yote nchini na kuwezesha wananchi kupata huduma bora za afya.

## Wafanyabiashara wawachongea wenzao kwa kukwepa VAT

**Na Alex Sayi,** MASWA

WAFANYABIASHARA wilayani hapa mkoani Simiyu wamewalalamikia wafanyabiashara wa jumla kwa kugoma kuwapa stakabadhi baada ya kuwauzia bidhaa kwa kisingizio cha kukwepa makato ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Wafanyabiashara hao walitoa malalamiko yao juzi, katika kikao na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wilayani hapa.

Mfanyabiashara, Charles Chagu alidai kuwa, wanakumbana na kadhia hiyo zaidi katika maduka ya vifaa vya ujenzi na vipuli vya magari ya jijini Mwanza.

"Tunashangaa tunaponunua bidhaa Mwanza ukiomba stakabadhi unaambiwa kama hutaki kununua acha ukifuatilia sana unaambiwa tatizo ni VAT sasa unajiuliza kwa nini wanakwepa kutoa stakabadhi kama hiyo VAT haina shida kama ambavyo (TRA) wanaizungumzia," alidai Chagu.

Mfanyabiashara mwingine, Zakaria Abel, alidai kadhia hiyo inawafanya waonekane wanakwepa kulipa kodi kwa kukosa nyaraka halisi wanapokaguliwa na maofisa wa TRA.

Abel aliiomba TRA kuendelea kuwaelimisha wafanyabiashara nchini umuhimu wa kulipa kodi na kutoa sitakabadhi kwa wateja.

Meneja TRA Maswa , Lucius Theonist, aliwaomba wafanyabiashara hao kuendelea kutunza kumbukumbu zao za biashara ili kuwasaidia maofisa wa mamlaka hiyo kufanya makadirio sahihi.

Theonist aliwataka wafanyabiashara hao kuwa na uzalendo kwa kulipa kodi na kuachana na tabia za ukwepaji kwa kuwa ni takwa la kisheria ili taifa liweze kujiendesha.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Aswege Kaminyoge akizungumza na wafanyabiashara hao, alisema ni vyema kutii sheria kwa kulipa kodi bila kusubiri kulazimishwa.

**Abel aliiomba TRA kuendelea kuwaelimisha wafanyabiashara nchini umuhimu wa kulipa kodi na kutoa sitakabadhi kwa wateja.**

Ukurasa 12



**Kijiji kilichokosa daraja tangu uhuru sasa chakumbukwa**

Ukurasa 13



**TGNP na kampeni nyumba kwa nyumba kuhamasisha kutoa maoni dira 2050**



DIRA 2050

# Ujenzi miji, vijiji ni holela kupindukia, iwekwe mikakati na viwango endelevu

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

KWA mgeni anayetembelea Tanzania kwa mara ya kwanza, akishuka kwenye ndege, meli, au basi, anachokiona ni makazi duni, holela na yasiyopangika kila upande atakaotupa jicho.

Ujenzi huo duni na holela wa makazi unaopatikana kuanzia mijini hadi vijijini, ni dosari inayotajwa na mbobezi wa kusanifu majengo Profesa mstaafu wa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU), Victor Chissanga.

Anasema:'Tanzania is growing too informaly in," akimaanisha ujenzi wa makazi ni holela kupindukia.

Anasema miji yote kuanzia Dar es Salaam ambalo ni jiji kuu hadi vijijini hakuna mipango na hilo ni janga kwa sababu hivyo kuwa nchi isiyozingatia mipango ya miji wala vijiji.

"Tukumbuke miaka 50 ijayo vijiji vyetu vitakuwa miji mikubwa au midogo. Miji nayo itakuwa majiji. Mbona hatujali kanuni za mipango mijini na vijijini. Tunakwenda wapi?" Anahoji.

Anaeleza kuwa miji kukosa mpangilio inasababisha kwanza kuwa na sura mbaya na kuongeza shinikizo la ziada au 'presha' kufikisha huduma muhimu na za kimsingi kama maji, umeme, barabara na mawasiliano.

Anasema majiji, miji mikuu, midogo na vijiji vinakuwa kiholela kiasi cha kushangaza wakati kuna wasomi wa mipango mijini na vijiji, wabunifu na wasanifu majengo wengi, wasio na kazi wakiachwa kuendesha bodaboda na kuuza mafuta ya magari vituoni au kufuga kuku.

"Jiji kuu la Dar es Salaam, majiji ya Arusha Mwanza, Mbeya na Tanga hayana mpangilio wa makazi, ujenzi holela unafanyika



Sehemu ya ujenzi holela kwenye Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

kwa kasi. Ni vyema kuchukua hatua. Kupanga sehemu za makazi, nyumba za aina tofauti, ghorofa fupi, ndefu, makazi ya viongozi, huduma za biashara, maduka, suparmarket, nyumba za ibada, shule na hospitali. Miji na vijiji visiachwe kukua kama uyoga au vinavyotaka vyenyewe."

Anasema sehemu ambazo hazijapangwa zipangwe serikali isitegemee kufanya 'upgrading ' au kuboresha, kunakohusisha kuvunja, kubomoa na pia kufidia hatua ambayo ni gharama zaidi.

Anatoa mfano makanisa kuibuka popote mijini yakijengwa kwa viroba, maturubai na mabati machakavu katikati ya miji na majijini bila kuona Idara ya Mipango Miji na Vijiji ikichukua hatua.

Profesa Chisanga anatoa mfano wa kujenga kiholela mabanda ya biashara popote mchuuzi anapotaka, lakini pia kuna vibanda vya kuuza simu, nguo, vinywaji na pombe juu ya mitaro ya barabara.

Anasema ndani ya hifadhi ya barabara kumewekwa vibanda vya mama na babalishe popote pembeni ya barabara kuu za majiji na miji na vibanda na nyumba zisizopangika na za kienyeji mno.

Anataja gereji, makontena ya kuuza pombe na bidhaa nyingine mtu anapoamua yanabandikwa popote na kuongeza: "Tunajiuliza hivi maofisa mipango miji na vijiji pamoja na idara ya upimaji wa ardhi na ramani wanachukuliaje hali hiyo?"

Profesa Chisanga aliyefanyakazi Chuo Kikuu cha Ardhi na vyuo vikuu vingine anakumbusha kuwa miji na vijiji visiyopangwa leo 2024 ndiyo majiji, miji mikuu na midogo ya kesho hivyo Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, iwajibike.

**UPIMAJI ARDHI**

Mtaalamu huyo anasema wananchi wanataka kujenga lakini hakuna ardhi iliyopimwa na hiyo ndiyo sababu ya kujenga kiholela, kuanzia Dar es Salaam hadi vijijini.

Anakumbusha kuwa Tanzania ni ya kwanza kuwa na chuo kikuu cha ardhi katika ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika lakini inashangaza kuwa ni nchi inayoongoza kwa makazi holela, duni na ukosefu mkubwa wa mipango miji na vijiji.

Makazi ya binadamu yana ngazi saba kwa Tanzania ikianza na majiji, miji mikuu ya mikoa miji mikuu ya wilaya, makazi ya tarafa, kata vijiji na vitongoji, anaeleza.

"Inashangaza ngazi zote ni ujenzi holela ambao hauzingatii mipangilio kuanzia barabara, usafirishaji, huduma za kijamii, miundombinu ya kibiashara na matumizi bora ya ardhi." Anasema msomi huyo.

"Inasikitisha kuanzia jiji kuu 'mega city' Dar es Salaam hadi kitongoji kilichoko mpakani Tunduma havijapangwa. Kuna wasomi wa mipango miji, wachora ramani, wasimamizi wa makazi na wasanifu majengo hawaajiriwi. Wapate kazi watimize jukumu hilo." anaongeza.

**ELIMU ITOLEWE**

Violate Mafuwe ni mbunifu wa majengo, anayefanyakazi Dar es Salaam, anasema kukosekana mipango miji na vijiji ni tatizo la kitaifa akishauri kupanga kuanze sasa.

Hata hivyo, anasema kabla ya yote elimu ya mipango miji na vijiji elimu itolewe ili watu wafahamu umuhimu, kisha washirikiane na mamlaka na Wizara ya Ardhi na Makazi kupanga maeneo yao.

"Watu wanatakiwa kuelimishwa athari za makazi holela, duni na namna ya kuyaepuka. Iwafikie wote walioko mijini na vijiji na waelezwe kuhusu sheria na kanuni zake."

Msanifu huyo anasema licha ya kwamba upangaji miji ulikosewa au kukosa kipaumbele miaka mingi iliyopita ni vyema kuanza sasa kutumia wataalamu kupanga na kuboresha makazi mijini na vijijini.

Viollet anashauri kuwa na vijijini vyenye mpangilio wa makazi,

INAENDELEA UK. 12

# Kijiji kilichokosa daraja tangu uhuru sasa chakumbukwa



Mto Mwandile unaotarajiwa kujengewa daraja. **PICHA: JUMBE ISMALY**

**Na Jumbe Ismaily, SINGIDA**

MOJA ya sababu zinazochangia kupanda gharama za maisha ya wananchi ni uharibifu wa miundombinu ya barabara, madaraja na vivuko kila wakati wa msimu wa mvua, iwe masika au vuli.

Pamoja na kupanda gharama za maisha vile vile husababisha baadhi ya huduma za kijamii kama afya, elimu kukosekana, au kutokupatikana kwa urahisi huku wajawazito na watoto wakipoteza maisha wakati wa kujifungua.

Kijiji cha Ntumbi wilayani Manyoni Mkoa wa Singida ni miongoni mwa maeneo ambayo tangu uhuru hayajawahi kubaki salama.

Changamoto haziishii hapo wengine wanasombwa na maji wakijaribu kuvuka mito kuwahi hospitalini.

Hata hivyo juhudi zimeanza kuwakwamua na kuwaondoa wasiwe maeneo yasiyofikika kirahisi kutokana na kuharibika kwa daraja la Mto Mwandile.

Tayari kwa mujibu wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Manyoni, serikali imetenga Shilingi milioni 415 kwa ajili ya daraja jipya litakalojengwa katika Mto Mwandile.

Taarifa za TARURA wilaya zinasema daraja hilo litakapokamilika litawanufaisha wananchi kwa kuwarahisishia upatikanaji wa huduma za kijamii.

Akiwa katika ziara za kukagua miradi ya maendeleo ya kata ya Nkonko, diwani wake Ezekiel Samwel, anashuhudia ujenzi wa daraja la Mto Mwandile unaoendelea, kuwaondolea adha wananchi wa eneo hilo.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Nkonko na Ntumbi, wanasema changamoto zilizokuwa zikiwakabili kwa kukosa usafiri wa uhakika kukosa fedha na kupanda gharama za maisha kutokana na bei za bidhaa kuwa juu.

Wanasema ujenzi wa daraja hilo linalojengwa na mkandarasi mzawa, utawaondolea kero ya ukosefu wa usafiri na kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na wananchi.

Wanavijiji hao wanaipongeza serikali kwa mradi huo wa kuwaboreshea miundombinu hasa barabara na daraja ambao utaunganisha kata za Nkonko, Sanza, Iseke na makao makuu ya wilaya ya Manyoni.

Wanapongeza kwa kuwaangalia wakijiita kuwa ni watu wa hali ya chini ambao wanaathirika kwa kukosa barabara na madaraja yanayopitika wakati wote wa mwaka.

John Mnyama mkazi wa Kijiji cha Nkonko anasema tangu uhuru mwaka 1961 wananchi wa vijiji vya Ntumbi na Ipanduka hawakuwa na miundombinu bora ya barabara, hivyo kupata shida kufikia huduma za kijamii kama hospitali na masoko.

Mnyama anawaasa wanufaika wa daraja hilo kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali ambayo imetoa fedha kwenye miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.

Mhandisi mjenzi wa daraja hilo, James Malisa anasema mradi wa daraja la Nkonko -Ntumbi una awamu mbili ambazo ni kipande cha Nkonko Ntumbi na kingine kipo upande wa Itagata, lakini kwa sasa wanaanza na ujenzi wa daraja.

Anasema mradi huo uliosainiwa Mei mwaka huu utakapokamilika utagharimu Shilingi milioni 415 na unatarajiwa kukamilika Novemba mwaka huu.

Anatoa wito kwa watumiaji wa daraja hilo kwamba baada ya kukamilika kwake walitunze kwa sababu serikali imewekeza fedha nyingi katika ujenzi wa daraja hilo.

Diwani wa Kata ya Nkonko, Ezekieli Samweli anasema wanufaika wakubwa wa daraja hilo ni wanakijiji cha Ntumbi chenye wakazi takribani 8,000.

Anasema kutokana na kutopitika kwa barabara hiyo gharama za vitu madukani zimepanda na kusababisha ugumu wa maisha kwa wananchi, hususani wakazi wa Ntumbi pamoja na vijiji vya kata jirani ya Iseke.

Diwani wa Viti Maalumu (CCM) Tarafa ya Nkonko, Rehema Chuji, anasema kabla ya kuanza kujengwa kwa daraja hilo, kulikuwa na changamoto kwa kinamama siku za kujifungua maji yanapokuwa yamejaa kwenye mto huo walikuwa wanahangaika kupita.

Kata ya Nkonko ina kituo cha afya kinachotegemewa pia na wanakijiji cha Ntumbi kupata huduma za afya kilichopo Nkonko na inapofika masika, kina mama wanaokwenda Nkonko wanakutana na changamoto mara nyingi na hata wengine kupoteza maisha.

Mwaka 2023 kuna mama alipoteza maisha akitokea Ntumbi kwa ajili ya kufuata huduma ya kujifungua katika kituo cha afya Nkonko.

Aidha, mwaka 2022 kina mama wawili na baba mmoja walipofika kwenye mto huo walizama.

Pamoja na hayo maharusi wawili waliokuwa wametoka kufunga ndoa walipozama wakati wakipita kwenye mto huo.

Wawili hao walisombwa na maji na hivyo kupoteza maisha, Rehema akitoa wito kwa wanaotumia barabara na daraja, hususani wakazi wa Ntumbi, Nkonko na Mwandile waendelee kutunza miundombinu hiyo.

Anawataka wafanyakazi wa kujitolea, washirikiane na mkandarasi mjenzi kwenye eneo la mradi kwa ajili ya kutengeneza daraja madhubuti.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Manyoni, Stephen Nyanda, anasema wilaya hiyo inahitaji takribani Shilingi bilioni 18 kukamilisha changamoto za miundombinu yote ya barabara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Manyoni, Annastazia Tutuba, anasema ujenzi wa daraja hilo utafungua mawasiliano na kurahisisha wakulima wa mazao ya biashara katika kata hiyo kutoka na kuingia ndani na nje ya kata hiyo.

Baadhi ya mazao yanayouzwa na wanavijiji wa kata hiyo ni karanga, ufuta, alizeti, mbaazi pamoja na asali.

## UJENZI MIJI, VIJIJI NI HOLELA KUPINDUKIA, IWEKWE MIKAKATI NA VIWANGO ENDELEVU

**INATOKA UK. 11**

serikali ibainishe ardhi au inunue kabla haijapanda thamani ianze kuweka alama za miundombinu ya mabomba ya maji, nguzo za umeme, gesi, mkongo wa taifa na hifadhi ya barabara.

Kadhalika ipange makazi kwa kuzitambulisha sehemu za kujenga nyumba za viongozi, nyumba za kisasa zaidi, za gharama nafuu, hospitali na vituo vya afya, shule, masoko, majosho ya vijiji, matangi ya maji, dampo za taka, viwanda, maeneo ya wazi na nyumba za ibada.

"Ni vyema kuwa na maofisa mipango miji na vijiji wasimamie kufikia ujenzi wenye viwango kwani maendeleo ya vijiji na miji yasipo simamiwa yana athari kimazingira."

Anakumbusha kuwa Tanzania ina ardhi ambayo haijaguswa bado akitaka ipangwe kabla ya kuchukuliwa na kupanda zaidi thamani.

### DIRA IWEKE VIWANGO

Erasmus Kiwango ni msanifu na mbunifu wa majengo, anayezungumzia umuhimu wa taifa kuandaa mpango endelevu wa ukuaji na upangaji miji na vijiji.

Anashauri dira ya taifa 2050 ianishe suala hilo na lifanyiwe kazi kama juhudi zinavyofanyika kujenga barabara, madaraja na reli na kufikisha maji na umeme kwenye makazi.

"Dira iweke viwango maalumu vya ujenzi na ukuaji wa miji na kuwe na utashi wa kisiasa kutimiza hatma hiyo," anasema Kiwango.

Anazungumzia kujenga miji mipya nje ya majiji iliyopangika yenye huduma zote ili kuondoa msangamano unaotokana na ujenzi holela wa majiji na miji mikuu.

Anasema miji hiyo inaweza kujengwa mikoa jirani kama Tanga na Pwani kupunguza msongamano Dar es Salaam.

Akiita 'setilite cites' kiwango anashauri katika maeneo hayo yawekwe masoko makubwa kama Kariakoo, hospitali za kitaifa na za rufani za kikanda, benki na chochote muhimu ili kuepusha kukifuata kwenye jiji.

Aidha, anasema kuwe na huduma za usafiri kuanzia miundombinu ya barabara na reli ili kuwapo na treni na mabasi ya mwendokasi, kielimu viwepo vyuo vikuu na shule za aina mbalimbali na makazi ya kila aina ya nafuu au juu zaidi.

Kiwango anasema makazi hayo ni kwa ajili ya wafanyakazi wa majiji ili waishi nje ya jiji lakini waweze kuwahi kazini na kurudi makwao muda wote.

Anashauri suala hilo lianze kufanyiwa kazi kupunguza msongamano Mwanza, Arusha, Dodoma na Tanga.

Kiwango cha Mkurugenzi wa kampuni ya ujenzi ya ECOSKY Builders ya Dar es Salaam, anasema pia ni bora kujenga miji kama Kibaha, Bagamoyo, Kigamboni na Chalinze na kuipa huduma muhimu ni suluhisho kupunguza msongamano na makazi holela.

"Ili kuwa na miji na vijiji vilivyopangwa ni lazima kushirikisha wananchi kwa sababu ardhi inamilikiwa na watu au mtu mmoja mmoja hivyo wanahitaji elimu kuelewa umuhimu wa kuruhusu ardhi hiyo kupangwa na kuwa na makazi bora," anashauri.

Hata hivyo anasema Dira ya Maendeleo 2050 iweke kipaumbele kuwa na mipango endelevu ya mipango na ukuaji miji na vijiji.

Anasema idadi ya watu inapoongezeka huduma nazo zitahitajika hivyo ni lazima kuzipanga na kuziwekea maeneo ya kuziweka.

# TGNP na kampeni nyumba kwa nyumba kuhamasisha kutoa maoni dira 2050

**Na Halfani Chusi, aliyekuwa KONDOA**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP), haupo nyuma kupinga ukatili wa kijinsia mara hii ikipenyeza ajenda kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025-2050, kulifanikisha ajenda usawa.

Mtandoa huo ukitumia tamasha la siku tatu lililotamatika hivi karibuni wilayani Kondoa Dodoma kufikisha ujumbe serikalini ili dira ijayo itokomeze ukatili wa kijinsia.

Katika tamasha hilo, Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Utafiti na Uchambuzi wa Mtandao huo, Zainabu Mmari, anasema uchambuzi wa mtandao umebaini Dira ya Maendeleo 2025 inayomalizika wananchi wengi hawakuifahamu.

Anafafanua kuwa wengi hawakushirikishwa katika mchakato wa kutoa maoni na pia hawakuielewa wakati wa utekelezaji wake lakini safari hii kasoro hiyo haipo.

Anasema dira 2025 kuna upungufu mkubwa wa kijinsia ambao umejitokeza maeneo matano yaliyowekwa kama vipaumbele vya dira.

"Upungufu uliokuwapo ni wananchi wengi kukosa uelewa kwamba hiki tunachokifanya ndicho kinakwendakutekeleza dira kufikia yale maisha bora tuliyoambiwa."

"Hivyo, mwisho wa siku tulikuwa tunatekeleza bila kuelewa tunafanya nini ili kufikia malengo tuliyoahidiwa," anasema Zainabu.

Anafafanua kuwa katika tamasha hilo wameangalia pia kwa kiasi gani makundi yote katika jamii hususani wanawake na wale wanaoishi pembezoni walipata fursa ya kushirikishwa katika mchakato wa maandalizi ya dira.

Anasema licha ya kwamba kuna mafanikio yaliyofikiwa katika maeneo kadhaa, kuna udhaifu mkubwa na pengo la kijinsia ambalo limejitokeza katika maeneo matano ambayo yaliwekwa kama vipaumbele vya dira akitolea mfano maeneo ya kijinsia hayakupewa kipaumbele kikubwa.

Anasema changamoto nyingine waliyoibaini ni kutokuwapo kwa viashiria vya kupima dira hiyo hasa kwenye masuala ya jinsia.

Zainabu anasema kutokana na changamoto hiyo kubwa TGNP inaendelea kuweka mkazo na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutoa maoni katika dira inayoandaliwa.

"Mpaka sasa tumeelimisha wananchi wengi kuelewa dirainayomalizika, lakini kuhimiza kuweka maoni yao kwenye dira mpya pia kufuatilia kuona kuwa yanachukuliwa ili kuwa na Tanzania wanayoitaka katika miaka mingine 25 inayokuja itakapofika 2050," anasema Zainabu.

Mratibu wa Vituo vya Taarifa na Maarifa vinavyoendeshwa kwa pamoja na wananchi, asasi za kiraia na TGNP kutoka Kata ya Ukenyenge Mkoa wa Shinyanya, Fredina Saidi, anasema namna walivyoshirikishwa kwenye kutoa maoni wanajamii wamejengewa ufahamu na kujamini.

Anasema kupitia ushirikishwaji unaofanywa na TGNP wameelewa namna gani wanaweza wakatoa maoni hususani mambo ambayo yanawahusu kwenye, usawa wa kijinsia, afya, maji, elimu miundombinu pamoja na usalama wa watu wote.

"Sisi wanajamii tuna jukumu kubwa la kuangalia matatizo na upungufu ambao tunao, tutoe maoni kuhusu mambo gani tunatamani yawepo ndani ya mpango huo mkubwa wa kimaendeleo," anasema.

## UELEWA WANANCHI

Katika tamasha hilo, Nipashe inafanya mazungumzo na wakazi wilayani huko na kubaini wengi wao hawana uelewa kuhusu dira ya taifa ya maendeleo na ukatili wa kijinsia, pia maadhimio ya miaka 30 ya mkutano wa Beijing.

Viktoria Ikandilo anaiomba serikali kuongeza nguvu kukabili vitendo hivyo ikiwamo kutoa elimu na kuweka sheria kali.

"Kesi nyingi zinamalizwa kifamilia kwa kuwa kuna jamii hazina uwelewa wa masuala ya ukatili wa kijinsia.

"Ndiyo maana kuna watoto wengi wa mitaani, wameathirika kisaikolojia, wimbi kubwa la ulawiti kwa kuwa ni vitendo vinavyoanzia zaidi majumbani na wazazi wengi hawakemei kwa sababu hawajui madhara yake," anasema.

Anasema tamasha hilo limeleta tija katika kuelimisha na kuhamasisha jamii, serikali na wadau kuwekeza nguvu na kutoa adhabu kali.

Aidha, anasema: "Hatujui nini maana ya dira ya maendeleo ya taifa, tunaona meseji kwenye simu tunazifuta hatujui inamaanisha nini tunaona kama zile za matapeli tu. Anasema tamasha hilo litaleta tija katika kuelimisha na kuhamasisha jamii, serikali na wadau kuwekeza nguvu na kutoa adhabu kali.

Mkazi mwingine Veronika Nganguli anasema tamasha hilo litahamasisha mwamko kwa makundi yote ili yatoe maoni kwenye diara ya taifa 2050.



Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Llundi. **PICHA: HALFAN CHUSI**

"Hasa ni kutoa maoni katika masuala ya nafasi za uongozi, uchumi, afya, elimu pamoja na kukumbushia malengo ya mkutano wa Beijing uliokuwa umelengea kueneza vuguvugu la usawa kati ya wanawake na wanaume.

"Mkutano huo uliofanyika China mwaka 1995 ulichochea ukombozi wa wanawake angalau kwa sasa wameshika nafasi katika sekta nyingi za uongozi japo hakuna usawa ukilinganisha na wanaume," anasema.

Mkazi mwingine Mariamu Mungayi, anasema katika wilaya hiyo wananchi wanauelewa mdogo kuhusiana na masuala ya ukatili wa kijinsia na mifumo dume. Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Lihundi, anasema wataendelea kutekeleza malengo ya Beijing kwa kushirikiana na mashirika yanayotetea haki za wanawake na usawa wa jinsia nchini.

Anasema pia wataendeleza vuguvugu la kuwashawishi wanawake kuwania nafasi za uongozi ili wajitambue na waondokane na manyanyaso.

Anabainisha kuwa lengo la kupeleka tamasha hilo Kondoa ni kutokana na takwimu kuonyesha wilaya hiyo bado ina tatizo la ukatili unaoendelea siku kwa siku.

"Tunafahamu kwamba changamoto ya mimba za utotoni ni kubwa wilayani Kondoa, wengi hawafahamu nini maana ya dira ya taifa ya maendeleo, lakini ni jambo linalohitaji juhudi kubwa kuanzia jamii na serikali."

Anasema Mkuu wa Wilaya, Fatma Nyangasa, anasema ni changamoto na kwamba anafanya tathmini ya kina ili kuandaa mikakati ya kuukabili.

"Ni matatizo ambayo kwa kiasi kikubwa yamejikita katika mila na desturi na yanahitaji nguvu za pamoja kufikia dira ya maendeleo ya mwaka 2050 mimba za utotoni iwe historia," anasema Lilian.

Kinachosemwa na Lilian kinaungwa mkono na mshauri mwelekezi katika masuala ya jinsia, sanaa na maendeleo, Agness Lukanga.

Akiwa na la ziada kwamba katika miaka 30 iliyopita tangu mkutano mkuu wa Beijing, upo uelewa mkubwa kuhusu masuala ya kijinsia. Ingawa matukio ya ukatili wa kijinsia yameongezeka, kasi ya kuripoti matukio hayo pia imeongezeka.

Agnes anasema kutokana na uelewa uliopo na sauti zinazopazwa, hatua mbalimbali zimechukuliwa na hata serikali imetengeneza mkakati wa kwanza wa kupinga na kupambana na ukatili.

Anakumbusha kuwa licha ya kuwapo kwa mwamko mkubwa wa kupaza sauti, bado kuna changamoto ambazo serikali inatakiwa kuzifanyia kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Fatma Nyangasa, anawataka wananchi kuitumia vema elimu waliyoipata kupitia tamasha hilo, lenye ujumbe 'dira jumuishi ya 2050, miaka 30 Beijing tujipange'.

## HAMKANI SI SHWARI TENA

# Somalia ‘mtu kati’ vita Misri, Ethiopia kugombea maji Nile

**Na Moshi Lusonzo**

MZOZO unaofukuta kati ya Misri na Ethiopia kuhusu uhalali wa matumizi ya maji ya Mto Nile, umeongeza hofu ya kuibuka vita baina ya mataifa hayo.

Misri imeiwashia Ethiopia taa nyekundu baada ya kusogeza vikosi vya majeshi Somalia na kuongeza sintofahamu.

Ikumbukwe Somalia inapakana na Ethiopia upande wa kaskazini, hivyo Misri kuanza kusogeza vikosi vyake eneo hilo kunaleta taharuki ukanda wa Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika.

Ni wasiwasi wa tishio la kuibuka kwa ushirikiano wa kijeshi kati ya Somalia na Misri unaoongeza hasira kwa Ethiopia ghadhabu inayoweza kuwa zaidi ya vita.

Mvutano huo uliongezeka karibuni baada ya kuwasili kwa ndege mbili za kijeshi za Misri aina ya C-130 katika mji mkuu wa Somalia, Mogadishu, kuashiria mwanzo wa makubaliano yaliyotiwa saini mwezi uliopita.

Mpango huo unahusu Misri kuwapeleka wanajeshi 5,000 kujiunga na kikosi kipya cha Umoja wa Afrika (AU) mwishoni mwa mwaka huu, huku wengine 5,000 wakiripotiwa kupelekwa katika mpango mwingine tofauti.

Ethiopia, ambayo huko nyuma ilikuwa mshirika muhimu wa Somalia katika kupambana na wanamgambo wenye mafungamano na al-Qaeda, iko katika mgogoro na Misri baada ya kujenga bwawa kubwa kwenye Mto Nile, jambo ambalo Misri inapinga.



Abdel Fattah el-Sisi Rais wa Misri



Hassan Sheikh Mohamud Rais wa Somalia



Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed

**ETHIOPIA MTEGONI**

Somalia licha ya kumleta karibu adui wa Ethiopia ambao wako vitani kupigania maji ya Nile, pia amepigilia msumari mwingine kwa kutangaza kwamba vikosi vya Ethiopia ambavyo viko nchini humo havitakuwa sehemu ya kikosi cha AU kuanzia Januari mwakani.

Kuna wanajeshi 3,000 wa Ethiopia chini ya ujumbe wa sasa wa Umoja wa Afrika, kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters.

Waziri Mkuu wa Somalia anasema Ethiopia italazimika kuondoa wanajeshi wake wengine kati ya 5,000 na 7,000 waliowekwa katika maeneo kadhaa chini ya makubaliano tofauti ya nchi hizo mbili, kama haitajiondoa katika mkataba wa kumiliki bandari walioafikiana katika jimbo la Somaliland.

Mtafiti mwandamizi kutoka Taasisi ya Royal United Services, Christopher Hockey, anasema hatua hiyo haitakubaliwa na Ethiopia ikiamini kuondolewa kwa wanajeshi wao kutaifanya nchi yake kuwa katika hatari ya kushambuliwa.

Anaiambia BBC kuwa kupelekwa vikosi vya Misri katika mpaka wake wa upande wa mashariki pia kutaifanya Ethiopia kuwa na wasiwasi.

Mkanganyiko huo ambao sasa umeleta hofu, unatokana na wazo la Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, ambaye anataka nchi yake ambayo haina bahari kuwa na bandari yake.

Ethiopia ilipoteza bahari wakati ilipotengana na Eritrea mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Waziri Mkuu Abiy anaitia saini mkataba wenye utata na Jamhuri ya Somaliland iliyojitangazia uhuru wake kutoka Somalia, kukodi sehemu ya kilomita 20 sawa na maili 12 ya pwani yake kwa miaka 50 ili kuanzisha kambi ya kijeshi.

Anadaiwa kwenda mbali kwa kuonyesha nia ya kuitambua rasmi Somaliland kama nchi huru, kitendo ambacho kimeikasirisha Somalia.

Somaliland ilijitenga na Somalia zaidi ya miaka 30 iliyopita, lakini Somalia inatambua kama sehemu ya eneo lake.

**CHANZO BWAWA**

Tatizo inalopelekea nchi hizo kutishiana lilianza 2011 baada ya Ethiopia kuamua kujenga bwawa kubwa la Grand Ethiopian Renaissance (GERD) katika mto wa Blue Nile.

Bwawa hilo linategemea kuchukua zaidi ya asilimia 85 ya maji yake katika mto huo.

Misri, ambayo inategemea maji ya mto Nile kwa asilimia 80, imekuwa na hofu kuwa bwawa hilo litaathiri mfumo wa usambazaji maji na pia kuifanya Ethiopia kuwa na mamlaka juu ya usambazaji wa maji ya Nile ambao ni mrefu kuliko yote barani Afrika ukiwa na kilometa zaidi ya 6,000.

Muda utakaotumika kujaza maji katika bwawa hilo unaweza kuleta upungufu mkubwa wa maji Nile.

Ethiopia inasisitiza ni lazima kukamilisha mradi wake wa bwawa na kueleza itajaza maji kwa miaka sita.

Misri ilipendekeza kipindi cha miaka 10 ili kutoa nafasi maji kutiririka katika hali yake ya kawaida na kuepuka athari za ukame katika maeneo yake.

Mazungumzo kati ya Misri, Sudan na Ethiopia kuhusu kuendesha mradi huo wa bwawa yamekwama kwa miaka minne na sasa, huku Marekani ikijaribu kuwapatanisha bila mafanikio.

Misri inasema Ethiopia iliendelea kujenga mradi huo kwa nguvu na kupuuza maslahi na haki za nchi nyingine kwa matumizi ya maji na usalama wao.

Pia ilidai kuwa kupunguzwa kwa asilimia mbili ya maji kutoka mto Nile kunaweza kusababisha kupotea kwa karibu hekari 200,000 za ardhi za kilimo cha umwagiliaji.

**HOFU YA WENGI**

Misri inaona ushirikiano wake wa kijeshi na Somalia kama kete ya kuilazimisha Ethiopia kuachana na mradi wake wa bwawa.

Rais wa Misri, Abdul Fattah al-Sisi, anaona kuweka kikosi chake cha kijeshi Somalia kutaleta suluhu ya mgogoro huo.

Dk. Hassan Khannenje, ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Kimataifa ya Mafunzo ya Mikakati ya Pembe ya Afrika anasema mgogoro huo utasababisha mapigano kati ya Ethiopia na Misri ikiwa vikosi vyao vitakutana katika mpaka wa Somalia.

Somaliland pia imeonya kuwa kuanzishwa kwa kambi za kijeshi za Misri ndani ya Somalia kunaweza kuyumbisha eneo hilo.

Dk. Khannenje anaiambia BBC kwamba iwapo mzozo utazuka, huenda ukaathiri zaidi matumizi ya Bahari ya Shamu na biashara ya kimataifa.

Misri imepewa nguvu na mkataba wa kikoloni wa mwaka 1929 ambao Uingereza ilitoa haki kwa nchi hiyo kumiliki na kukataza kazi zozote zinazoweza kuhatarisha utiririshaji wa maji ya mto Nile.

Pia Misri ilipewa haki ya matumizi ya mita za ujazo bilioni 55.5 kati ya bilioni 84 ya maji ya mto Nile.

Misri ilikuwa na haki ya kutembelea na kuchunguza kila mahali mto huo unapopita na miradi inayofanyika ili kuulinda.

Hata hivyo, mwaka 2010 nchi nne za Afrika Mashariki na Kati zilisaini mkataba mpya wa matumizi ya maji ya mto Nile, huko Uganda na kuutengua ule wa awali ulioandaliwa na mkoloni.

Nchi zilizotia saini mkataba huo mpya ni Tanzania, Uganda, Kenya Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Rwanda na Burundi.

Misri na Sudan ambazo zinatumia maji ya mto huo kwa kiwango kikubwa zilishiriki katika majadiliano, lakini zilipinga vipengele vyote 15 vilivyomo katika mkataba huo mpya.





## RC: Sitaki kuwaona maofisa ugani 'mnambwela' mbwela mjini

**Na Elisante John,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego ametoa onyo kali kwa maofisa ugani kuacha kufanya kazi kwa mazoea na kuwaamuru wanaoishi mjini kurudi vijijini kwenye maeneo walikopangiwa na serikali kufanya kazi.

Akizungumza juzi kwenye hafla ya kukabidhi vishikwambi kwa wataalamu wa ugani kwa ajili ya matumizi na usimamizi wa masuala ya kilimo, Dendego alisema lazima maofisa ugani wazingatie wajibu wao.

Alisema uwekezaji katika kilimo unaofanywa na serikali hauwezi kufanikiwa bila ya kuwapo kwa wataalamu wazuri na makini katika kuboresha kilimo kwa ajili ya kuinua uchumi wa wakulima na wananchi.

Alisema baadhi ya maofisa ugani wamekuwa wakifanya kazi kwa mazoea na kuishi mbali na vituo vya kazi, na wengine kutovaa vazi rasmi la kazi, jambo ambalo linazorotesha juhudi za serikali kuboresha sekta ya kilimo nchini.

Alisisitiza kuwa, hataki kuwaona maofisa hao wakizurura mjini badala yake waishi kwenye maeneo yao ya kazi kama walivyopangiwa na serikali. "Nisiwaone mjini mnambwela mbwela tu, nataka kuwakuta wote kwenye vituo vyenu na kuishi huko huko kule mlikopangiwa, mbona mimi nipo hapa nimehamia Singida," alisema Dendego.

Alikemea tabia ya maofisa hao kila siku ya kazi kusafiri kwenda vijijini kwenye maeneo yao ya kazi na jioni kurudi mjini, akisema hali hiyo haikubaliki.

"Sitaki kuona mtaalamu au mkuu wa idara anakaa mjini wakati amepangiwa Ilongero kila siku anafukuzana na magari kuwahi kazini kijijini," alisema.

Vilevile, alikemea tabia ya baadhi ya maofisa kutumia vibaya vifaa kwa shughuli binafsi kwa kuwa wanazorotesha usimamizi wa shughuli za ugani kwenye maeneo yao

Baadhi ya maofisa waliokabidbiwa vishikwambi, akiwamo Natalia Mosha wa Halmashauri ya Wilaya Singida, alisema vitawasaidia kupata takwimu sahihi kuhusiana na masuala ya kilimo kwa wakati.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, aliwaeleza maofisa hao kuwa serikali ina nia ya dhati kuboresha kilimo na itachukua hatua madhubuti dhidi ya wanaokiuka usimamizi wa kilimo

# Kinamama kutengewa maeneo kunyonyesha watoto ofisini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kuweka maeneo ya kina mama kunyonyeshea watoto mahali pa kazi ili kuimarisha afya zao.

Mpango huo ulitangazwa juzi jijini hapa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima wakati wa mkutano mkuu wa kwanza wa Mtandao wa Wanawake Jeshi la Magereza Tanzania (TPSW-net).

Gwajima, alisema kwa maslahi mapana ya jamii, serikali imekuja na mpango huo ili kuhakisha kinamama wanyonyeshaji wanaondokana na kero ya kukamua maziwa kwa ajili ya kuwaachia watoto nyumbani.

Alisema, kuna haja Kamishna Jenerali wa Magereza kuangalia namna ya kuliweka suala hilo katika mipango ya taasisi hasa ujenzi wa miundombinu mipya.

Alisema kuwapo kwa chumba cha kunyonyeshea watoto mahali pa kazi kutaleta faida nyingi kwa mwajiri na mwajiriwa.

Gwajima, alisema kwa upande wa mwanamke aliyeajiriwa, itasaidia kutimiza wajibu wake ipasavyo na faida nyingine.

"Utaratibu huu utaongeza ari na uwajibikaji, pia utapunguza mahudhurio hafifu kazini.

Tukifanya hivyo itatusaidia pia wanawake wanaonyonyesha kupunguza kuomba ruhusa kazini kwa ajili ya kwenda kunyonyesha,"alisema.

Katika hatua nyingine Dk. Gwajima alisema anatarajia kuwasilisha sera ya mtandao huo Bungeni ili iweze kutungiwa sheria na kujulikana kwa jamii.

Alisema sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2023 inatoa dira ya usawa katika nyanja zote za maendeleo, hivyo nao wakijulikana, kutasaidia mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Alisema, mkakati wake wa mwaka 2023 unaonesha dhamira ya serikali kukuza usawa wa kijinsia kama njia mojawapo ya kuimarisha maendeleo ya watu na Taifa.

Mwenyekiti wa Mtandao huo, Kamishna wa Huduma za Urekebu wa Magereza, Bertha Minde, alisema mtandao huo ulianzishwa mwaka 2018.

"Huu ni mkutano wetu mkuu wa kwanza tunamshukuru Mkuu wa Jeshi la Magereza kwa kuwezesha kufanyika," alisema.

Alitaja baadhi ya madhumuni ya mtandao huo kuwa, ni kushirikiana na jamii kudhibiti uhalifu na ukatili wa kijinsia katika jamii.

Akisoma risala, Tekla Ngilangwa, alisema miongoni mwa mada zitakazojadilliwa ni itifaki, afya ya akili, uongozi na maadili, ujasiriamali, ukatili wa kijinsia, nidhamu na wajibu wa mwanamke katika jamii na sehemu ya kazi.

Nyingine ni nishati safi ya kupikia, mafao, wajibu wa haki za wanawake na watoto na sheria, kanuni na miongozo ya jeshi hilo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema miongoni mwa mada katika mkutano huo ni ukatili wa kijinsia ambao umekuwa changamoto katika jamii na kupelekea watoto kufanyiwa ukatili huku baadhi ya wazazi wakihusishwa.



Mbunge wa Viti Maalumu, Ester Matiko (kushoto), akimpongeza Mbunge wa Kigamboni, Dk. Faustine Ndugulile, kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika hivi karibuni, walipokutana Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kampeni kutokomeza utapiamlo kuzinduliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wa Jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zaidi ya 2000 wanakutana jijini hapa kujadili masuala mbalimbali ikiwamo uzinduzi wa kampeni ya kutokomeza utapiamlo nchini kwa watoto kutokana na lishe duni.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalum, Mwanaidi Ali Khamis wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Mwanaidi, alisema mkutano wa mwaka wa jukwaa hilo litafunguliwa leo na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko na kufanyika kwa siku tatu.

Alisema jukwaa hilo limeandaliwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) ili kuendeleza ushirikiano baina yake na serikali, sekta binafsi na washirika wa maendeleo.

"Jukwaa hilo limetanguliwa na majukwaa ya mashirika haya ngazi za wilaya na mikoa, yamefanyika majadiliano kuhusu fursa na changamoto katika utekelezaji wa shughuli za mashirika, mafunzo ya kujengeana uwezo, utambuzi wa mashirika yaliyofanya vizuri na maazimio ya kushughulikia changamoto zilizoibuliwa na wadau mbalimbali," alisema.

Alitaja shughuli zitakazofanyika kwenye jukwaa hilo kitaifa kuwa ni mafunzo kwa wasajili wasaidizi na wajumbe wa NaCoNGO wa mikoa, uzinduzi wa madawati ya uratibu wa mashirika katika sekta binafsi na mjadala wa nafasi ya asasi za zisizo za serikali (NSAs) katika uboreshaji wa huduma za afya nchini.

Vilevile, alisema kutakuwa na mafunzo kuhusu usimamizi wa miradi, uandishi wa maandiko dhana ya miradi, uandishi wa taarifa ya mfadhili na ufuatiliaji, programu za huduma za kijamii kupitia dhana ya uwajibikaji kwa jamii (CSR) na Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC) katika eneo la Nkuhungu, Chamwino na Chang'ombe.

"Septemba 6, 2024 itakuwa kilele cha jukwaa la mwaka huu, ambapo baadhi ya shughuli zitakazofanyika siku hiyo ni uzinduzi wa Kampeni ya Kutokomeza Njaa na Utapiamlo kwa Watoto, ambao utatanguliwa na matamko ya wizara za kisekta,"alisema.

Meneja Uchechemuzi na Jinsia kutoka Shirika la World Vision, Ester Mongi, alisema kampeni ya utapiamlo kwa watoto kutokana na lishe duni itaanzia mikoa 16 ya Tanzania Bara.

"Tunashirikiana na wizara tano tukiamini kabisa wadau wote waliopo katika mikoa ambayo sisi hatupo wataenda kufanya ambacho sisi tunakifanya, "alisema na kuongeza kuwa: "Kampeni hii itadumu kwa miaka mitatu."



# Halmashauri yabanwa ilipe wazabuni, watumishi mabilioni

**Na Agustino Kihombo,**
IRINGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Iringa mkoani hapa imetakiwa kuwalipa shilingi bilioni 4.7 wazabuni ili kujenga imani ya kuendelea kutoa huduma mbalimbali.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Ofisa Usimamizi wa Fedha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa, George Sangai katika kikao cha baraza la madiwani cha halmashauri hiyo kwa ajili ya kupokea taarifa ya fedha ya mwaka 2023/2024 iliyoishia Juni 30, mwaka huu.

Sangai, alisema kutokana na ongezeko hilo la madeni, ni vyema halmashauri ikaweka utaratibu wa kulipa ili kupunguza mzigo na kuchochea maendeleo ya wananchi.

Alisema halmashauri hiyo inadaiwa na wazabuni ambao wamekuwa wakitoa huduma kwa halmashauri kiasi cha sh. bilioni 1.2, kitendo ambacho kinaweza kusababisha kukosa imani nayo, hivyo kushindwa kuendelea kufanya kazi.

"Hii tukiacha iendelee ni hatari sana tutapoteza imani kwa watoa huduma wetu ni lazima tuone namna ya kulipa haya madeni," alisema Sangai.

Kwa upande wa watumishi, alisema mpaka sasa wanadai shilingi milioni 968 na kuitaka halmashauri kuweka mikakati wa kulipa madeni hayo ili kuongeza morali kwa kada hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Steven Mhapa, alisema halmashauri imeweka mchanganuo wa kutambua kiwango cha madeni na wanaowadai ili kuwalipa madai yao.

Baadhi ya madiwani, akiwamo Methwe Nganyagwa na Fundi Mihayo, walisema ni wajibu wa kila diwani kuhakikisha anasimamia ukusanyaji wa mapato katika eneo lake ili kuongeza mapato ya halmashauri hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24 imekusanya zaidi ya asilimia 93. Hivyo, jitihada zinahitajika ili kuongeza zaidi mapato na kufikia asilimia 100 kwa mwaka wa fedha 2024/2025.




Meneja Mkuu wa Ura Saccos, ACP Kim Mwemfula (wa pili kulia), akibadiliashana mkataba na Meneja Masoko wa Kampuni ya Alaf, Isamba Kasaka, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuingia makubaliano ambapo Saccos hiyo itatumia bidhaa za kampuni hiyo. Kushoto ni Mkuu wa Biashara wa Kampuni hiyo, Sateesh Yamsani na Mjumbe wa Bodi ya Ura Saccos, Christopher Mwambona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shule zaagizwa kuanzisha klabu kupinga ukatili

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka ameziagiza shule za msingi na sekondari mkoani hapa kuanzisha klabu za maadili na kupinga ukatili wa kijinsia ili kuwajengea uwezo wanafunzi kutambua mabaya yanayoweza kuwakuta katika jamii.

Mtaka alitoa agizo hilo juzi katka uzinduzi wa kampeni ya Jeshi la Polisi ya "Tuwaambie kabla Hawajaharibiwa" uliofanyika viwanja vya Sabasaba mjini hapa.

Alisema klabu hizo zitakuwa na majukumu kama zilivyo klabu za wapinga rushwa na mazingira.

Aliviagiza vyombo vya usalama kuchunguza taarifa zote kuhusiana na ukatili kwa watoto ili kupata ukweli.

"Nitazungukuka kwenye shule tufanye hii kampeni kuhusu suala la maadili, kuhusu suala la ukatili wa kijinsia sio jambo la kuweza kufumbia macho, utayasikia kwa mtoto wa mwenzio kesho yatakuja nyumbani kwako," alisema.

Mtaka, alisema lazima kutengeneza kizazi salama kwa kutambua hatari ya ukatili wa kijinsia na matendo mabaya ambayo yanatokea katika jamii.

**Shilogile alisema, utekelezaji wa kampeni hiyo unatarajia kuleta mafanikio kwa watoto watakaoanza sekondari na vyuo kuwa na uelewa wa dhana nzima ya kujitambua.**

Kamishna wa Polisi Dawati la Jinsia, Maria Nzuki, alisema kampeni hiyo inalenga kuwaelimisha watoto kujilinda dhidi ya ukatili wa kijinsia kabla hawajapatwa na madhara.

Kamishna wa Polisi Jamii Tanzania, Faustine Shilogile, alisema utandawazi kwa asilimia kubwa umesababisha mmomonyoko wa maadili kwa watoto na matukio mengine ya kikatili.

Shilogile alisema, utekelezaji wa kampeni hiyo unatarajia kuleta mafanikio kwa watoto watakaoanza sekondari na vyuo kuwa na uelewa wa dhana nzima ya kujitambua.

Baadhi ya wanafunzi, akiwamo, Ahimidiwe Mligo, alisema wanapaswa kujiepusha na vitendo hatarishi vya kupokea zawadi toka kwa watu wasiowafahamu.

## Kiwanda cha kuchakata ngano kujengwa Makete

**Na Elizabeth John,**
MAKETE

BARAZA la madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete mkoani Njombe, limepitisha azimio la kujenga kiwanda cha kuchakata ngano katika Kijiji cha Kimani Kata ya Mfumbi ili kuinuia kipato cha mkulima wa zao hilo.

Azimio hilo lilipitishwa katika kikao cha baraza hilo cha kupokea taarifa za maendeleo ya kata cha robo ya nne kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kilichofanyika juzi mjini hapa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe, aliliambia baraza hilo kujengwa kwa kiwanda hicho kitakachokuwa na uwezo wa kuchakata tani 50 kwa siku, kutaondoa kero nyingi ikiwamo ngano ya wakulima kukosa soko la uhakika

"Ili kufanikisha jambo hili tayari halmashauri imetenga shilingi milioni 64 na kiwanja cha ekari tisa chenye hati, kilichopo Kijiji cha Kimani; sambamba lazima tuwe na uhakika wa malighafi na shamba lenye ukubwa wa ekari 1000 la ngano pia," alisema Makufwe.

Kabla ya kupitisha mpango huo, baadhi ya madiwani, Abel Mahenge, Sainel Nyambo na Gwerino Mwasanga, walisema uanzishwaji wa kiwanda hicho utakuwa na manufaa kwa halmashauri na taifa. Hivyo, wanaunga mkono suala hilo.

"Ubunifu huu wa mkurugenzi utawapa watu nguvu za kuweza kulima na hatutakuwa tunahangaika tena kwenda kununua ngano sehemu nyingine kwa sababu itakuwa inatosheleza," alisema Mahenge.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Christopher Fungo, alisema ujenzi wa kiwanda hicho kutawasaidia wakulima kupata soko la uhakika na kipato cha uhakika.

Awali Halmashauri hiyo ililiomba baraza hilo liridhie kuundwa kwa kampuni itakayosimamia uendeshaji wa kiwanda hicho, kukopa shilingi bilioni 2 kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) na kusajiliwa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) kwa lengo la kunufaika na misamaha ya kikodi.



## Wavuvi waomba msaada wa boti wavue kisasa

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

WANACHAMA wa kikundi cha uvuvi cha 'Nyange Cooperative' Mjiniole Wilaya ya Chakechake Pemba wameiomba serikali kuwapatia boti ya kisasa itakayowawezesha kuvua samaki wengi na wakubwa ili wakajikwamue kiuchumi.

Walisema tayari wamepeleka maombi ya kupatiwa boti ya mkopo kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa, ingawa hadi sasa hawajapewa licha ya kukumbushia kila baada ya muda.

Wakizungumza na Nipashe kisiwani hapa, walisema wamekuwa wakivua samaki bila ya mafanikio, hali ambayo imewadumaza.

Mmoja wa wavuvi hao, Hamad Khatib alisema walisema walitarajia kupatiwa boti, itakayowasaidia kupata samaki wengi na wakubwa, ambapo wangeweza kukuza soko na kujipatia kipato.

"Samaki tunaopata hawakidhi mahitaji yetu na pia ni wadogo, hivyo tunavua na tunapata pesa kidogo tu ya chakula, hivyo tunakosa huduma nyingine muhimu," alisema.

Hamad alisema waliomba boti ya mita nane lakini hawajapewa na tayari wameshafungua akaunti ya benki kama walivyoagizwa, ingawa wanaendelea kusubiri.

Mwanachama mwingine, Hadia Ali Hamad, alisema lengo la kuanzisha kikundi chao ni kujikomboa na umaskini ingawa bado hawajafika malengo kutokana na kukosa nyenzo muhimu za kuvulia.

Ofisa Mdhamini kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba, Dk. Salim Mohamed Hamza, alisema wizara ikipokea maombi mbalimbali ya wavuvi kutaka boti na wao huyapeleka katika Benki ya CRDB.

Alisema, benki hiyo ndiyo yenye mamlaka ya kuyaangalia maombi ya wavuvi na kupima vigezo walivyoviweka, kwamba vinastahili kwa kikundi kupatiwa mkopo wa boti za uvuvi au havistahili.

Alisema Serikali ya Zanzibar iliikabidhi fedha CRDB baada ya kupokea mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha Duniani (IMF) ili kupunguza athari za kiuchumi baada ya kujitokeza kwa mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Kikundi hicho kina wanachama 24, wanawake 17 na wanaume saba, ambapo wana miradi mbalimbali ikiwamo ya uvuvi, ufugaji wa samaki, uhifadhi wa mazingira, pamoja na kulima mboga na matunda.

# Wizara ya Ujenzi kuendana na mageuzi ya kidunia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imesema imejipanga kuendana na mageuzi ya kidunia inayoendana na sekta ya ujenzi.

Hivyo, imeanza kufanya mapitio ya sera na sheria kwa kushajihisha usajili wa wahandisi na kampuni za ujenzi ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Habiba Hassan Omar, wakati akifunga Kongamano la Miaka 50 la Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Karume (KITS) Zanzibar.

Alisema hatua hiyo itaimarisha usimamizi wa utoaji wa huduma bora na kupatikana ujenzi bora na salama.

"Tutasimamia hili kwa maadili ya kitaalamu na kuweka viwango bora vya ujenzi na kufuatilia utekelezaji wake ipasavyo. Na katika kufanya kazi hii tutaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo taasisi ya jumuiya za wahandisi, wasanifu majengo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na taasisi zote zinahusika na ujenzi Tanzania," alisema.

Hivyo, aliwataka wahandisi kujijenga kimaadili kwa kuheshimu taaluma zao na kuepukana na matendo na tabia zinazokwenda kinyume na maadili ya kazi zao.

Aidha, aliwataka kuepuka na vitendo vya rushwa, kuitia hasara serikali na wateja wao kwa kuwa na usanifu, ukadiriaji na usimamizi bora wenye viwango vinavyohitajika na gharama zinazostahiki.

Pia alitaka kufanyike ushajihishaji wa watoto shuleni hasa watoto wa kike kupenda kusoma masomo ya sayansi ili kujiunga na masomo ya juu katika fani mbalimbali za uhandisi.

Dk. Habiba alisema kwa mujibu wa takwimu Zanzibar kuna wahandisi 361, kati yao wanawake ni 75, hivyo bado kuna safari ndefu za kuleta uwiano wa kijinsia katika fani ya uhandisi na teknolojia.

Mmoja wa washiriki hao, Fatma Kara, alisema uhandisi ni fani muhimu, kwamba kukua kwa sekta ya utalii kumefungua fursa nyingi ikiwamo ya ujenzi wa majengo ya hoteli za kitalii.

Alisema ni muhimu fani hiyo ikisomewa na jinsia zote na KITS kiendelezwe zaidi ili sekta ya ujenzi isaidie maendeleo ya nchi.

Fatma alisema Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Salmin Amour Juma ndiye aliyefungua milango ya wahandisi wanawake Zanzibar kutambulika, kwamba yeye ni miongoni mwa wanufaika hao.

Alisema katika uongozi wa Rais huyo kulijengwa jengo la Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) eneo la Kinazini ambalo sasa linatumika kwa ofisi za Umoja wa Mataifa (UN).

Alisema na yeye (Fatma) alikuwa miongoni mwa wahandisi waliopata nafasi katika ujenzi wa jengo hilo na kuanza kuaminika na kushiriki katika majengo mengi ndani na nje ya Zanzibar.



Mhandisi wa majengo wa kwanza mwanamke kwa Zanzibar, Fatma Kara, akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa kongamano la miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Chuo cha Sayansi ya Teknolojia Karume, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Miongozo, sera za watu wenye ulemavu hazitoshelezi'

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Abeida Rashid Abdallah, amesema miongozo na sera inayohusu watu wenye ulemavu haitoshelezi.

Amesema ipo haja ya kuangalia sera na sheria zingine namna ilivyowajumuisha watu hao, ili kuhakikisha hakuna kundi ambalo limeachwa nyuma katika jamiii.

Alisema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa Programu ya Kimataifa ya Haki za Watu Wenye ulemavu, uliyofanyika visiwani Zanzibar.

Alisema Sera ya Mwaka 2004 inayohusu watu wenye ulemavu haitoshelezi, hivyo ipo haja ya kuangalia sera na sheria zingine namna ilivyowajumuisha kundi hilo.

Alisema watu wenye ulemavu wanalazimika kupaza sauti zao kwa kuieleza jamii changamoto zinazowakabili kutokana na upungufu uliopo kwenya sera na sheria.

Aidha alisema muda wowote kuanzia sasa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itazindua mpango kazi wa kitaifa wa kumpambana na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kwamba umezingatia masuala ya watu wa kundi hilo.

Pia alizitaka jumuiya za watu wenye ulemavu kuweka takwimu zao ingawa serikali imeweka takwimu, lakini ni vyema na wao wenyewe kuweka takwimu zao vizuri ili ziweze kuwasaidia wakati wa kutoa maoni yao.

Kadhalika, alizipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongoza na Rais Samia Suhuhu Hassan na Serikali ya Zanzibar inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinnyi kwa uongozi wao pamoja na kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia na masuala ya watu wenye ulemavu.

Mtaalamu wa ushauri wa masuala ya usawa wa kijinsia, Maja Hansen, alisema mkutano huo umelenga kuzungumzia ajenda nne ikiwamo ushiriki na ushirikishaji, ulinzi wa vitendo vya ukatili kwa watu wenye ulemavu.

Baadhi ya washiriki wa mkutano huo, Ali Omar Makame kutoka Shirikisho la Jumuiya la Watu Wenye ulemavu Zanzibar (SHIJUWAZA) alisema amefurahishwa na hatua ya waandaaji wa mkutano huo namna walivyowashirikisha watu wenye ulemavu katika kikao hicho.

Alisema hatua hiyo itawawezesha kueleza changamoto zinazowakabili ikiwamo ukosefu wa vyoo rafiki kwa baadhi ya majengo ya serikali na binafsi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LILIAN JOSEPH** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0611- 0516 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KABANGA HIGH SCHOOL mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **KBA/PS//B.2/29/VOL.XXV/**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**GRENA SILVESTER AINEA** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE040162** iliyotolewa uhamiaji makao makuu DAR ES SALAAM PCO mnamo tarehe 26/07/2018. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/25688/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACKLINE KESSY NYANGASA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 0766-0024,** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIMAMBA SECONDARY SCHOOL mwaka 2009.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi **POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/25688/2024**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 17848 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU MUSTAFA HAIDI MKULO**
**KHALIDA AKBARY MKULO......MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**( Kanuni ya 75)**

Watu wote wanodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kudika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 23 mwezi 09, 2024 , saa 08:00 asubuhi. Siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe . A.A Omari .
Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 13 mwezi 08, 2024

NAIBU MSAJILI

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 19259/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late MUSSA PETER LUKUMAY of SWASWA**
**Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**ELIZABETH PETER LUMAY AND ABRAHAM RYOBA MORA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 04 Day of 09, 2024
Date at Dodoma this 20TH Day of JULY, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 173 YA MWAKA 2024**
**BAINA YA**

**JUDITH KANJE ........................................ MDAI**

**DHIDI YA**

**JAPHARY MUSA ..................................... MDAIWA**

**KWA:**
**JAPHARY MUSA**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 02.10.2024 saa 3:00 asubuhi kwa ajili ya kutaja.
**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 03 ya mwezi Septemba, 2024.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA TANZANIA

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(DODOMA SUB REGGISTRY)**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 18955 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late HELEN STEPHEN MBEBA**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION OF THE DECEASED ESTATE BY HASSAN MAULID MOHAMED**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 12th Day of September, 2024

Dated at Dodoma this 19th Day of August, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

**THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**TEMEKE HIGH COURT SUB – REGISTRY**
**(ONE STOP CENTRE)**
**AT TEMEKE**

**PC. CIVIL APPEAL NO.16795 OF 2024**

**FARIDA ISSA LUKANGA...........................APPELANT**

**VERSUS**

**ANISA CHIWANGO...............................RESPONDENT**

**TO: ANISA CHIWANGO**
**DAR ES SALAAM**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above appeal has been fixed for hearing on 10TH SEPTEMBER, 2024 at 9:00 A.M before **Hon. S. S. SARWWATT, judge.**
You are required to appear in this court without failure. In default of your appearance on the day before mentioned, the appeal will be heard and determined in your absence
GIVEN under my hand and seal of the court this 29 AUGUST, 2024

DEPUTY REGISTRAR

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Biden, Kamala Harris wafanya kampeni pamoja

**NEW YORK, Marekani**

RAIS wa Marekani Joe Biden na makamu wake Kamala Harris wamefanya kampeni ya pamoja kwa mara ya kwanza huko Pennsylvania tangu Biden alipojiondoa katika kinyang'anyiro cha kuwania urais wa taifa hilo.

Ilielezwa jana kuwa Rais Biden na makamu wake Kamala walionekana wakiwa pamoja kwenye kampeni juzi, huku wadau wa kisiasa wakisema tukio hilo linaonesha umoja tangu Kamala alipochukua nafasi ya Biden kama mgombea wa Chama cha Democratic katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 5, mwaka huu.

Ilielezwa kuwa viongozi hao wawili wamehudhuria hafla ya kuadhimisha siku ya wafanyakazi Marekani pamoja na wanachama wa shirikisho katika jimbo lenye ushindani mkali katika uchaguzi la Pennsylvania.

Pia ilibainishwa kuwa kabla ya hafla ya pamoja na Biden huko Pennsylvania, Kamala aliuhutubia umati wa watu mjini Detroit, jimboni Michigan, akitafuta kuimarisha uungwaji mkono wa vyama vya wafanyakazi na wapigaji kura wa tabaka la wafanyakazi ambao mgombea wa chama cha Republican Donald Trump anadai ni ngome yake.

Rais Biden, mwenye umri wa miaka 81, alijiondoa kutoka kwenye kinyang'anyiro cha kuwania urais mwishoni mwa mwezi Julai mwaka huu chini ya shinikizo kubwa lililokuwa likiongeza, kutokana na kufanya vibaya katika mdahalo dhidi ya mpizani wake Donald Trump.

Hata hivyo, hatua yake ya haraka kumuidhinisha na kumuunga mkono makamu wake Kamala, mwenye umri wa miaka 59, kulimsaidia kupata uungwaji mkono wa chama cha Democratic na kuteuliwa rasmi kama mgombea wiki chache baadaye.

*DW*



Mtoto wa Rais wa zamani wa Afrika Kusini Momcebo Zuma kushoto aliyechumbiwa na Mfalme wa Eswatini, akiwa na baba yake Jacob Zuma. **PICHA: MTANDAO.**

# Mahututi kwa kuchomwa moto na mpenzi wake

**NAIROBI, Kenya**

MWANARIADHA wa Uganda wa mbio za marathon Rebecca Cheptegei (33) yuko katika hali mahututi katika hospitali moja nchini Kenya, baada ya kudaiwa kumwagiwa petroli na kuchomwa moto na mpenzi wake wa zamani, huku sababu za tukio hilo zikiwa bado hazijajulikana.

Kwa mujibu wa taarifa ya polisi iliyotolewa jana, mwanariadha huyo ambaye alishiriki katika michezo ya Olimpiki yaliyofanyika siku chache zilizopita huko Paris, amepata majeraha ya moto ya zaidi ya asilimia 75 katika mwili wake.

Taarifa ya polisi ilisema Rebecca alishambuliwa nyumbani kwake magharibi mwa Kenya ambako alikuwa akifanya mazoezi, na kwamba kuna wasiwasi kuhusu ongezeko la visa vya ukatili dhidi ya wanariadha wa kike nchini humo, ambavyo baadhi vimesababisha vifo.

"Rebecca anasemekana kuokolewa na majirani baada ya mpenzi wake wa zamani kudaiwa kumwagia petroli na kumchoma moto nyumbani kwake katika mji mdogo wa Endebess," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kamanda wa Jeshi la Polisi katika eneo hilo Jeremiah Kosiom, ilisema mtu anayedaiwa kuwa mshambuliaji pia alipata majeraha mabaya katika kisa hicho kilichotokea Jumapili, na kwamba walisikika wakizozana nje ya nyumba yao.

Pia alisema wawili hao wamelazwa katika hospitali ya rufaa ya Moi mjini Eldoret, mji mkuu wa eneo hilo. Huku ikielezwa kuwa wakati wa ugomvi huo, mtuhumiwa alionekana akimmiminia mwanamke huyo mafuta kabla ya kumchoma.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Rebecca kutoka eneo lililo karibu na mpaka na Uganda, anasemekana kununua kipande cha ardhi katika kaunti ya Trans Nzoia na kujenga nyumba, ili kuwa karibu na vituo vingi vya mafunzo ya riadha nchini Kenya.

Ripoti iliyowasilishwa na msimamizi wa eneo hilo ilisema kwamba wawili hao walikuwa wakizozana kuhusu kipande hicho cha ardhi. Huku polisi wakisema uchunguzi kuhusu kisa hicho unaendelea.

Vile vile, ilielezwa kuwa Aprili 2022, mwanariadha mwingine wa kike, Damaris Mutua, alipatikana akiwa amenyongwa nyumbani huku akiwa amefunikwa usoni na mto wa kulalia katika mji wa Rift Valley wa Iten.

Hatua hiyo ilijiri miezi kadhaa baada ya mwanariadha aliyevunja rekodi ya mbio ndefu Agnes Tirop kupatikana akiwa amechomwa kisu hadi kufa katika mji huo huo.

Desemba 2023, mwanariadha mwingine wa Uganda, Benjamin Kiplagat aliuawa kwa kuchomwa kisu na wavamizi huko Eldoret.

*BBC*

# Binti wa Jacob Zuma achumbiwa na Mfalme Mswati III

**CAPE TOWN, Afrika Kusini**

BINTI wa Rais wa zamani wa Afrika Kusini Jacob Zuma ni miongoni mwa mamia ya wanawake na wasichana waliocheza ngoma kwa ajili ya Mfalme wa Eswatini katika sherehe za kitamaduni juzi, kuthibitisha uchumba wake na mfalme huyo.

Binti huyo ambaye ni Nomcebo Zuma (21), alikuwa miongoni mwa watu 5,000 kutoka katika ufalme huo mdogo katika sherehe maarufu kama ‚Reed dance' ya kila mwaka katika Kijiji cha Kifalme cha Ludzidzini huko Lobamba, kusini mashariki mwa mji mkuu Mbabane.

Ilielezwa kuwa japokuwa sherehe hiyo ya siku nzima ni ya kitamaduni kwa mwanamke, imefanyika wakati ambako Mfalme Mswati (56), anaweka wazi chaguo lake la mke mpya.

Tayari ana takriban wake 14, baadhi yao aliwaoa walipokuwa wadogo, na ana takriban watoto 25.

Aidha, wiki iliyopita, kaka yake Mswati alisema kuwa Nomcebo Zuma atahudhuria ngoma ya Reed kama „liphovela", ambayo ina maana ya mchumba wa kifalme.

Katika hafla ya jioni ya Jumatatu, alikuwa miongoni mwa mamia ya wasichana waliovalia mavazi ya kitamaduni, wengine wakiwa na mapanga na ngao za kuigwa, ambao walicheza mbele ya Mswati na msafara wa wanaume waliovalia ngozi za kitamaduni.

Baba yake Jacob Zuma (82), pia ana wake wengi kutokana na mila zao na watoto takriban 20. Alilazimika kujiuzulu kama rais wa Afrika Kusini 2018 chini ya wingu la tuhuma za ufisadi.

*TRT*

**Ilielezwa kuwa japokuwa sherehe hiyo ya siku nzima ni ya kitamaduni kwa mwanamke, imefanyika wakati ambako Mfalme Mswati (56), anaweka wazi chaguo lake la mke mpya.**

# DABO YAMETIMIA AZAM, IBENGE ATAJWA KUMRITHI

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane**

BAADA ya tetesi za muda mrefu, hatimaye Klabu ya Azam, imetangaza rasmi kuachana na Kocha wake Mkuu, Youssouph Dabo, aliyedumu kwenye kikosi hicho kwa muda wa mwaka mmoja, huku ikidaiwa huenda nafasi yake ikajazwa na Florent Ibenge wa Al Hilal ya Sudan.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na klabu hiyo imeeleza kuwa wamefikia makubaliano ya pande mbili kutoendelea kufanya kazi pamoja kuanzia jana Septemba 3.

"Bodi ya Wakurugenzi ya Azam FC na Kocha Dabo, wamefikia makubaliano ya kutoendelea kufanya kazi pamoja kuanzia leo, Septemba 3, 2024.

"Dabo aliyehudumu kwenye klabu hii kwa kipindi cha mwaka mmoja, anaondoka na wasaidizi wake wa benchi la ufundi aliokuja nao.

"Klabu, pamoja na wadau wake inapenda kumshukuru Dabo kwa weledi na moyo wake wa kutokata tamaa katika kipindi chote alichokuwa nasi na tunamtakia kila laheri huko aendako," ilieleza taarifa hiyo na kuongeza:

"Wakati Bodi ikiwa kwenye mchakato wa kutafuta kocha mpya, programu za timu zitakuwa chini ya makocha wa timu zetu za vijana."

Kocha huyo raia wa Senegal, anakuwa wa pili kutimuliwa kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara, ambapo wakwanza alikuwa ni Mkenya, David Ouma wa Coastal Union.

Hata hivyo, makocha wote hao wanatimuliwa si kwa sababu ya mechi za Ligi Kuu ambayo ndiyo kwanza ipo raundi ya pili, bali ni sababu za michezo ya kimataifa.

Wakati Ouma alitimuliwa kwa Coastal kutolewa kwenye Kombe la Shirikisho Afrika kwa jumla ya mabao 3-0 dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola, Dabo ilionekana hana maisha marefu ndani ya Azam, baada ya timu hiyo kuondoshwa kwenye hatua za awali, Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya APR ya Rwanda, kwa jumla ya mabao 2-1, ikishinda bao 1-0 nyumbani na kuchapwa 2-0 jijini Kigali.

Tetesi zinadai kuwa viongozi wa Azam wapo kwenye harakati za kumshamwishi kocha raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Ibenge wa Al Hilal kuchukua nafasi yake.

## VIPAJI ZAIDI...



Afisa Utamaduni, Sanaa na Michezo Wilaya ya Muheza, Tanga, Msafiri Nyaluva, akimkabidhi mipira mitatu mchezaji wa timu ya wanawake ya Economy Queens, Zubeda Ally, katika fainali ya Bonanza la Muheza Queens Soccer, iliyofanyika Uwanjani wa Shule ya Sekondari ya Wazazi ya Mbaramo juzi. Bonanza hilo lilidhaminiwa na Ofisi ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Wilaya ya Muheza likishirikisha timu nne ambazo ni Jambe Queens, Songa Queens, Sega Queens na Economy Queens ambazo zote zimepata zawadi ya mipira, lengo likiwa ni kuinua vipaji. Kulia ni Diwani wa viti maalum Muheza, Amina Mbawala. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Singida, Mwenda warushiana lawama

**Na Adam Fungamwango**

SAKATA la mchezaji Israel Mwenda na Klabu ya Singida Black Stars, limeendelea kuchukua sura mpya baada ya beki huyo wa pembeni kudai kuwa hawezi kwenda kambini na yupo kwenye hatua ya kuvunja mkataba.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mwenda alisema hawezi kwenda kambini kama Klabu ya Singida Black Stars inavyotaka, badala yake yupo kwenye mkakati wa kuvunja mkataba kwani hata pesa yenyewe waliompa, walifanya hivyo nje ya makubaliano.

Klabu ya Singida juzi ilitoa tamko la kumtaka mchezaji huyo kwenda kambini, na kuahidi kumlipa pesa zake anazodai akiwa kazini.

Klabu hiyo ilisema ilimpa mchezaji huyo aliyetoka Simba, Sh. milioni 140, na zilizobaki ni Sh. milioni 60, na kwa makubaliano yao angezipata akiwa tayari kambini.

"Subirini tu hivi karibuni mtapata majibu nipo kwenye harakati za kuvunja mkataba na mtapata ukweli. Mimi si mjinga nisiende kambini, hayo ya kwenda kambini na kulipwa Sh. milioni 60 yana undani wake, ngoja kwanza nimalize mambo yangu, pesa yenyewe nimelipwa nje ya mkataba tuliokubaliana.

"Si lazima kuendelea na hili, mimi nina pesa ya kutumia hata kama sitacheza kwa misimu minne," alisema mchezaji huyo.

Awali, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hussein Massanza, alisema wachezaji wote wa klabu hiyo walikuwa wameripoti kambini kasoro mchezaji huyo ambaye walimtaka kufanya hivyo haraka.

"Tangu tumetambulisha wachezaji wetu, Mwenda hajaripoti kambini na kimsingi, ni kweli kuna vitu alihitaji ili kurejea kambini ambavyo kwanza ni vipya, havipo kwenye mkataba.

"Makubaliano halisi ya mkataba sisi tumeshayatekeleza na sehemu iliyobaki tulikubaliana yatafanyika mchezaji akiwa eneo lake la kazi, lakini ni kama amegoma hivi, anataka atimiziwe yote ndio aje kambini, hii imetusikitisha sana, ila bado tunaendelea kutumia busara ili mchezaji aje," alisema.

Habari zinasema kiasi cha pesa alizopewa awali alizitumia kuvunja mkataba wake Simba, na kilichobaki ndicho kingekuwa chake.

# Inter Zanzibar yazitaka pointi tatu za JKU SC

**Na Hawa Abdalla, ZANZIBAR**

TIMU ya Inter Zanzibar FC imesema mchezo wao wa kwanza dhidi ya Mabingwa Watetezi, JKU SC, haitaki kufanya makosa ili kuwa na mwanzo mzuri wa ligi hiyo.

Inter Zanzibar FC inashuka uwanjani Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa New Amaan Complex visiwani hapa majira ya saa kumi Alasiri dhidi ya JKU.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abraman Mohmed, alisema mipango yake ni kuhakikisha wanapata alama tatu katika mchezo wao wa kwanza wa na msimu wake wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema ingawa wanashuka uwanjani dhidi ya timu ngumu ambayo pia ni mabingwa watetezi wa ligi hiyo, lakini hakutowazui kutimiza lengo lao.

Mohmed alisema wameyatumia mapumziko yao vizuri hasa katika kukiboresha kikosi hicho kwa maingizo mapya na wachezaji wao wa zamani ambao waliipandisha daraja timu hiyo.

"Tumefanya maandalizi, si tu kwa ajili ya mchezo wa kwanza, lakini kwa michezo yote ya ligi ila mchezo huu wa kwanza tunatamani kupata alama tatu," alisema.

Aidha, alisema watashuka uwanjani kwa kuzingatia nidhamu na heshima kwa wapinzani wao kutokana na uzoefu walionao katika soka la Zanzibar.

"Ili tufanikiwe kupata ushindi, lazima tuzingatie kuwa tunaenda kucheza na timu ambayo kwanza ni bingwa mtetezi, lakini wana wachezaji wazuri na wenye uwezo wa kufanya chochote ndani ya uwanja," alisema.

Hata hivyo, aliwataka mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi katika mchezo huo ili kutoa hamasa kwa wachezaji kama ilivyokuwa msimu uliopita.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TRIPPIER AGOMBEWA UTURUKI

KLABU tatu za Uturuki, Fenerbahce, Besiktas na Eyupspor zote zina nia ya kumsajili mlinzi wa Newcastle, Kieran Trippier baada ya klabu ya Saudi Pro League Al-Ittihad pia kujaribu kumsajili mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 33. ***(Sky Sports)***

### MATIP ATAKIWA WEST HAM

WEST Ham inavutiwa na mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Cameroon, Joel Matip mwenye umri wa miaka 33 na mchezaji wa kimataifa wa Jamhuri ya Ireland, John Egan mwenye miaka 31, huku wakitafuta soko la wakala huru kumnunua beki mpya wa kati. ***(Sky Sports)***

### MAN UNITED YAMZUIA ERIKSEN

MANCHESTER United haiwezi kumruhusu kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 32 kuondoka mwezi huu. ***(Football Insider)***

### ELANGA AWANIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United itajaribu tena kumsajili winga wa Nottingham Forest mwenye umri wa miaka 22 kutoka Sweden, Anthony Elanga katika dirisha dogo lijalo la usajili. ***(Football Insider)***

### AJAX KUMSAJILI SULEMANA

AJAX imekubali kwa mdomo mkataba wa mkopo na Southampton kwa mshambuliaji wao wa miaka 22 raia wa Ghana, Kamaldeen Sulemana. ***(Fabrizio Romano)***

### LIVER, ARSENAL ZAMTAKA REIS

LIVERPOOL na Arsenal ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia kwa karibu beki wa kati wa Palmeiras mwenye umri wa miaka 18, Mbrazil Vitor Reis. ***(Caughtoffside)***

### EVERTON ILIWAKATAAA DISASI, FOFANA

KLABU ya Everton ilikataa pendekezo la kumsajili mlinzi wa Chelsea, Axel Disasi, mchezaji wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26, na fowadi wa Ivory Coast, David Datro Fofana mwenye umri wa miaka 21, katika makubaliano ya kubadilishana na mshambuliaji wa Toffees, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 27. ***(Givemesport)***

### NDALA MBIONI KUTUA EINDHOVEN

WINGA wa Manchester City, Joel Ndala mwenye umri wa miaka 18 anafanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kabla ya kujiunga na PSV Eindhoven kwa mkopo ikiwa na masharti ya kununua. ***(Athletic)***

### HAGI KUIKATAA BURCHAREST FCSB

MSHAMBULIAJI wa Romania, Ianis Hagi mwenye umri wa miaka 25 anatazamiwa kukataa nafasi ya kuondoka Rangers na kujiunga na Bucharest FCSB. ***(Football Insider)***

### ARMSTRONG KUHAMIA VANCOUVER

KIUNGO wa kati wa Scotland, Stuart Armstrong mwenye umri wa miaka 32, ambaye aliondoka Southampton mwishoni mwa msimu uliopita, anakaribia kuhamia Vancouver Whitecaps. ***(Daily Hive)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# OSIMHEN ATUA GALATASARAY

Waturuki hao wamekubaliana kumsajili kwa mkopo nyota huyo wa Nigeria baada ya...

**ISTANBUL, Uturuki**

GALATASARAY imemsajili mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen kwa mkopo, klabu hiyo ya Uturuki ya 'Super Lig' imetangaza.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria mwenye umri wa miaka 25 aliongeza mkataba na klabu hiyo ya Italia Desemba mwaka jana hadi 2026 kwa kipengele cha kuachiwa cha euro milioni 130.

Mwezi mmoja baadaye, Rais wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, alisema Osimhen ataondoka mwishoni mwa msimu huu, mshambuliaji huyo hakujumuishwa katika kikosi rasmi cha Napoli cha wachezaji 23 kwa ajili ya Serie A msimu huu.

Wakati msimu wa uhamisho wa majira ya kiangazi ulipokaribia kufungwa wiki iliyopita, ilionekana Osimhen huenda angetua Chelsea, lakini dirisha la usajili lilifungwa nchini Italia na England siku ya Ijumaa bila ya uhamisho kukamilika baada ya klabu hiyo ya Ligi Kuu kuripotiwa kutokuwa tayari kumsajili.

Uhamisho wa kwenda klabu ya Saudi Pro League, Al Ahli pia haukufaulu na kumwacha Osimhen katika sintofahamu.

Mabao 26 ya Osimhen yalisaidia Napoli kushinda Scudetto misimu miwili iliyopita, lakini wakapitia kipindi kigumu kuanzia hapo.

Dirisha la uhamisho nchini Uturuki litafungwa Septemba 18 na hiyo imepepeleka Galatasaray kufanikiwa kumsajili mshambuliaji huyo wakijiandaa kushiriki Ligi ya Europa msimu huu.

# SUAREZ ATANGAZA KUSTAAFU URUGUAY

**MIAMI,** MAREKANI

LUIS Suarez ametangaza kustaafu kuichezea timu ya taifa ya Uruguay, akisema ataondoka kwenye majukumu ya kimataifa baada ya mechi ya taifa hilo ya kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Paraguay Ijumaa hii.

Nyota huyo wa zamani wa Liverpool na Barcelona, ambaye sasa anaichezea Inter Miami katika Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS, anaondoka kama mfungaji bora wa muda wote wa Uruguay akiwa na mabao 69 katika michezo 142 wa kipindi cha miaka 17.

"Hakuna kujivunia zaidi ya kujua wakati sahihi wa kustaafu ni lini, na kwa bahati nzuri nina uhakika kwamba ninastaafu kutoka kwa timu ya taifa kwa sababu ninataka kujiweka kando," alisema Suarez akiwaambia waandishi wa habari.

"Nina umri wa miaka 37 na najua ni vigumu sana kufika Kombe lijalo la Dunia, inanifariji sana kwamba naweza kustaafu njia nyingine na si majeraha yanayonistaafisha, au kuacha kuitwa.

"Kwangu binafsi, inanisaidia sana kutaka kuchukua hatua hiyo kando na kujiona niko tayari. Ni ngumu kwa sababu uamuzi haukuwa rahisi. Lakini nakwenda nikiwa na amani ya moyo kwamba hadi mchezo wa mwisho nilijitolea kwa kila kitu, na kwamba mwanga haukuwaka polepole na ndiyo maana nilifanya uamuzi kwamba iwe hivyo sasa."



Suárez alicheza mechi yake ya kwanza kwa Uruguay Februari 8, 2007, katika ushindi wa 3-1 dhidi ya Colombia na hivi karibuni akawa sehemu muhimu ya kikosi.

Kufikia mwaka 2010, alishiriki katika mechi 19 kati ya 20 za kufuzu Kombe la Dunia ili kupata nafasi ya kikosi cha La Celeste kwenye mashindano hayo huko Afrika Kusini.

Fowadi huyo alikuwa sehemu muhimu ya kikosi katika Kombe lake la kwanza la dunia, akianza mechi tano kati ya sita za Uruguay.

Wakati wa robo fainali dhidi ya Ghana, Suarez aliudaka mpira kwa mikono katika dakika za mwisho za mchezo, na kuipa Ghana nafasi ya kushinda mchezo huo kwa penalti.

Licha ya Suárez kutolewa nje kwa kadi nyekundu, Asamoah Gyan alikosa penalti hiyo na Uruguay wakashinda mechi kwa mikwaju ya penalti na kutinga nusu fainali.

Suárez anaendelea kutetea hatua hiyo hadi leo, akiita „okoa bora zaidi ya mashindano."

Tangu wakati huo ameshiriki katika Fainali zingine tatu za Kombe la Dunia kuanzia mwaka 2014, 2018 na 2022 na vile vile Copa America ya 2011, 2016, 2019, 2021 na 2024.

Wakati wa fainali za 2011, fowadi huyo alifunga bao la ufunguzi katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Paraguay katika fainali ya Copa América ambayo iliweka taifa kwenye njia ya ushindi wake wa 15 wa mashindano makubwa.

Kwa jumla, aliweza kufunga mabao manne na pasi mbili za mabao mwaka huo na kupata tuzo ya mchezaji bora wa mashindano hayo.

"Nilikuwa na bahati kushinda mataji mengi katika kipindi changu cha uchezaji, lakini isingebadilisha taji la Copa América kwa chochote duniani," aliongeza Suarez.

"Hilo kombe la Copa América mwaka wa 2011 ulikuwa wakati mzuri zaidi nilioupata katika maisha yangu kama mchezaji wa kulipwa. Isingebadilisha kwa lolote na tazama, nilishinda vitu vingine vingi."

Suárez alijiunga na kikosi cha Miami kilichokuwa na nyota wengi, akishirikiana na Lionel Messi, Jordi Alba na Sergio Busquets, kabla ya msimu wa MLS wa 2024 na amekuwa akifanya vizuri.

Alifunga mara mbili katika mchezo wa mwisho wa Miami, ushindi wa 4-1 dhidi ya Chicago Fire FC, na kufikisha jumla ya mabao 16.

## Man United yamkingia kifua Ten Hag

**MANCHESTER,** ENGLAND

ERIK ten Hag anaungwa mkono kikamilifu na timu mpya ya uongozi ya Manchester United, kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu, Omar Berrada.

United ilimpa nyongeza ya mwaka mmoja kwenye mkataba wa kocha Ten Hag katika msimu wa majira ya joto.

Hiyo ilifanyika licha ya mmiliki mwenza wa United, Sir Jim Ratcliffe na Mkurugenzi wa michezo wa INEOS, Sir Dave Brailsford kutangaza baadhi ya watu wanaoweza kuchukua nafasi yake akiwemo Thomas Tuchel na Roberto De Zerbi.

Berrada na mkurugenzi wa michezo Dan Ashworth walianza majukumu yao mapya baada ya uamuzi wa kumpa Ten Hag mkataba mpya.

Lakini Berrada, ambaye alikuwa akizungumza kabla ya kufungwa 3-0 na Liverpool siku ya Jumapili, alisisitiza Mholanzi huyo anaungwa mkono na wakuu wa klabu.

"Tunafurahi sana na uamuzi huo kumpa Ten Hag mkataba mpya," alisema Berrada.

"Erik ana ufadhili wetu kamili na tumefanya kazi kwa karibu sana katika dirisha hili la uhamisho. Tutaendelea kufanya kazi naye kwa karibu kumsaidia kupata matokeo bora nje ya timu.

"Je, bado tunamwamini Erik? Kweli kabisa. Tunafikiri Erik ndiye kocha sahihi kwetu na tunamuunga mkono kikamilifu."

Licha ya kutokuwa na uhakika kuhusu nafasi yake kufuatia ushindi wa fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City Mei, Ten Hag amekuwa na mchango mkubwa katika kusajili wachezaji majira ya joto.

Takriban pauni milioni 200 zimetumika kununua wachezaji watano wapya wakiwemo Matthijs de Ligt, Noussair Mazraoui, Leny Yoro, Joshua Zirkzee na Manuel Ugarte.

Ten Hag, ambaye anaanza msimu wake wa tatu Old Trafford, alitoa wito wa uvumilivu baada ya kushindwa na Liverpool siku ya Jumapili.

Ashworth pia anakiri itachukua muda kuona matokeo, lakini amesema anafurahishwa na kikosi kilichokusanywa katika dirisha la kwanza chini ya uongozi wake.

"Ninakipenda kikosi, lazima niseme," alisema Ashworth.

"Pengine ningesema hivyo baada ya biashara tuliyofanya wakati wa kiangazi. Pengine nimefanya madirisha 25 sasa na nimekuwa nikifanya hivi kwa muda wa kutosha."

## Ronaldo yupo sana Ureno

**LISBON,** URENO

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo amepuuzia mbali maelezo ya uvumi kuwa amefikiria kustaafu kuichezea timu ya taifa katika siku chache zijazo, akiongeza kuwa ukosoaji wa baada ya Euro haukumtia wasiwasi.

Ureno itaikaribisha Croatia katika mechi ya kwanza ya Ligi ya Mataifa ya Uefa Alhamisi kabla ya kuikaribisha Scotland Jumapili, huku kocha Roberto Martinez akimtaja Ronaldo kwenye kikosi kwa ajili ya mechi hizo mbili.

"Hayo yote yametoka kwa vyombo vya habari. Haikuniingia akilini kwamba mzunguko wangu na Ureno ulikuwa umefikia kikomo," alisema Ronaldo katika mkutano na wanahabari.

"Kinyume chake kabisa, ilinipa motisha zaidi ya kuendelea kuwa mwaminifu na mpambanaji."

"Motisha ni kuja kwenye timu ya taifa kutwaa Ubingwa wa Mataifa ya Uefa....Tayari tumeshinda mara moja na tunataka kufanya hivyo tena. Ninaweza kusema jambo lile lile tena na tena."



Ronaldo aliongoza Ureno kwa mafanikio katika mchezo wa ufunguzi wa Ligi ya Mataifa ya Uefa msimu wa 2018-19, miaka mitatu baada ya kuwa Mabingwa wa Ulaya kwa mara ya kwanza huko Ufaransa.

"Mpaka mwisho wa kazi yangu, nitakuwa na mawazo kwamba nitakuwa naendelea kucheza," aliongeza Ronaldo.

"Ninachohisi kwa sasa, na maneno ya kocha Roberto Martinez pia yanaonesha hili, ni kwamba ninaendelea kuwa rasilimali kwa timu ya taifa, na nitakuwa wa kwanza kukubali kama hiyo sio kesi.

"Ninapokuwa sio tena mali nitakuwa wa kwanza kuondoka. Lakini nitaenda na dhamiri safi, kama kawaida, kwa sababu najua mimi ni nani, ninaweza kufanya nini, ninafanya nini na nitafanya nini."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39 alionekana kutosumbuliwa na shutuma alizokabiliana nazo kwa kushindwa kufunga bao kwenye michuano ya Ulaya 2024.

Pia alikosa penalti ya muda wa ziada katika hatua ya 16 bora nchini Ujerumani.

HABARI MICHEZO

# BENKI YA CRDB YAZINDUA MICHUANO SUPA CUP 2024

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imezindua rasmi msimu mpya wa mashindano ya soka na netiboli yajulikanayo kwa jina la CRDB Bank Supa Cup 2024.

Uzinduzi huo umefanyika jijini Dodoma jana katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya John Merlin, ukiongozwa na Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Fredrick Nshekanabo, pamoja na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, Godfrey Rutasingwa.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi, Nshekanabo alisema lengo kuu la mashindano hayo ni kuongeza ari, nguvu na ushirikiano baina ya wafanyakazi wa benki.

"Baada ya kusambaza tabasamu kwa wananchi wa Tanzania na kuvuka mipaka ya nchi na kwenda nchini DR Congo na Burundi, sasa ni zamu ya tabasamu hilo kurudi nyumbani kwa wafanyakazi," alisema Nshekanabo.

Alisema kuwa mashindano hayo yatashirikisha wafanyakazi wa Benki ya CRDB kutoka matawi mbalimbali, pamoja na makao makuu wakishindana vilivyo kugombania kombe la msimu.

Aidha, mashindano hayo yalienda sambasamba na programu ya kujitolea kwa wafanyakazi wa benki hiyo wakiongozwa na Mkurugeni wa Rasilimali Watu kutoa misaada ya vifaa vya kazi katika Hospitali ya Rufaa ya Dodoma, kuchangia damu, pamoja na kutoa chakula na vinywaji kwa wagonjwa hospitalini hapo.

Benki ya CRDB ilianzia programu hiyo maalumu ya wafanyakazi wake kujitolea mwaka huu ikilenga kusogea karibu kwa jamii wanayoihudumia.

Kwa upande wa Rutasingwa, alisema benki yao ni sehemu ya Jamii na ndiyo maana wamekuwa mara kwa mara wakishiriki katika program za kusaidia jamii. "Sisi kama Benki ya CRDB ni sehemu ya jamii na hatuna budi kurudi kwao kuchangia chochote kile ili kusogeza mbele maendeleo yetu.

„Programu hii ilizinduliwa visiwani Zanzibar mwezi uliopita na tunatarajia kuendelea kufanya hivyo katika mikoa mingine baada ya hapa Dodoma,“ alisema.



Wafanyakazi wa Benki ya CRDB wakipambana kwenye mchezo wa netiboli wa michuano ya CRDB Bank Supa Cup 2024, inayoendelea jijini Dodoma. **MPIGAPICHA WETU**

# JKT Queens kambini mapema kwa Ligi Kuu

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha msimu huu hakifanyi tena makosa kwenye mbio za ubingwa, Kikosi cha timu ya JKT Queens, kimeanza kambi mapema kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu ya Wanawake.

Msimu uliopita JKT Queens, ilipoteza taji la ligi hiyo dhidi ya Simba Queens, ambayo pia ilizoa alama zote sita dhidi ya miamba hiyo ya jeshi.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa timu hiyo, Masau Bwire, alisema wameamua kuanza kambi mapema ili msimu ujao wabebe ubingwa wa ligi hiyo.

"Huwa ni kawaida yetu kuanza maandalizi mapema kwa kuwa tuna malengo ya kufanya vizuri zaidi msimu ujao ili tubaki na ubingwa," alisema Bwire.

Aliongeza kuwa kikosi kipo imara kuhakikisha kinapata matokeo mazuri kwenye michezo yao yote watakayoicheza msimu ujao.

Aidha, alisema kutokana na aina ya wachezaji waliopo katika kikosi hicho ana matumaini makubwa ya kupata matokeo mazuri kwenye mechi zao ligi itakapoanza.

Alisema kabla ya msimu kuanza watacheza michezo ya kirafiki huku wakiwa wana subiri ratiba itolewe ili wajue wanaanza na nani.

Aliwataka mashabiki wao kuendeleakuwapa ushirikiano kama walivyofanyia msimu uliopita ili watimize malengo yao.

## Ateba: Nitafunga sana mabao Simba

INATOKA UK. 24

takuwa na furaha zaidi, ninachowaambia mashabiki wa Simba ni kwamba waje kwa wingi uwanjani kila tunapocheza kutushangilia, msimu huu tunataka kushinda tu, pamoja na kutwaa mataji, hakuna kingine,“ alisema straika huyo.

Ateba, ambaye alisubiriwa kwa hamu na wanachama na mashabiki tangu katika mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Tabora United na wa pili dhidi ya Fountain Gate na kushindwa kuonekana kwa sababu za vibali, alionekana kwa mara ya kwanza katika mchezo wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Al Hilal ya Sudan, Jumapili iliyopita.

Katika mchezo huo, aliwapa zawadi ya bao dakika ya 26, ambalo liliifanya timu hiyo kutoka sare ya bao 1-1, mchezo uliochezwa, Uwanja wa KMC uliopo Mwenge, Dar es Salaam.

Wakati huo huo, klabu hiyo imesema itakuwa na mchezo mwingine wa kirafiki, Jumamosi ijayo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema kuwa mchezo huo ni moja kati ya mapendelezo ya kocha Faldu Davids katika kukinoa kikosi kabla ya mchezo wake dhidi ya Al Ahly Tripoli.

Hata hivyo, hakuitaja timu watakayocheza nayo wala uwanja, akisema mambo yatakapokaa sawa, ataweka kila kitu hadharani.

## Stars na sababu za kuiua Ethiopia leo kufuzu Afcon

INATOKA UK. 24

tunaanza, tumejianda na kujipanga vizuri, tunataka kuanza vizuri safari yetu kuelekea kwenye fainali hizo huko Morocco,“ alisema Morocco.

Aliweka wazi kuwa wamefanikiwa kuwafuatilia katika michezo michache ya hivi karibuni kupitia mikanda ya video na hiyo imewasaidia kujipanga vizuri kuvuna pointi tatu.

"Ni muhimu sana sisi kama Tanzania kufuzu fainali za mwakani, tunajiandaa kuandaa fainali za mwaka 2027, itakuwa na maana kubwa sana tukifuzu fainali za Morocco,“ alisema kocha huyo.

Kwa upande wa mwakilishi wa wachezaji, Dickson Job, alisema wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo na kudai watapambana kwa asilimia 100 kuweze kupata pointi tatu.

"Kwa upande wetu sisi wachezaji, tumejipanga vizuri kuhakikisha tunafanya vizuri katika mchezo huu, lengo ni kuanza vizuri mchezo wetu wa kwanza,“ alisema Job.

Katika mechi tatu za mwisho za hivi karibuni, Stars haijapata ushindi mbele ya Ethiopia ikitoka sare michezo miwili na kufungwa mmoja.

Michezo
Jumatano Septemba 4, 2024
Nipashe

## Osimhen atua Galatasaray

UKURASA 21



# Ateba: Nitafunga sana mabao Simba

●●● Apania kufunika rekodi yake akiwa Ligi Kuu Cameroon, aitaka mechi Al Ahly Tripoli huku...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA mpya wa Simba, Leonel Ateba, ameahidi kufunga mabao mengi akiwa na klabu hiyo, akiwaambia mashabiki kuwa huu ni msimu wa ushindi na mataji tu, hakuna kingine wanachohitaji.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Ateba, alisema tofauti na watu wengi nchini wanavyomfikiria, kwake kufunga mabao ni jambo ambalo amelizoea, hivyo alishangaa kuona baadhi ya mashabiki wakiwa na wasiwasi naye.

Ateba, alisema kutokana na upendo na ushirikiano kutoka kwa wachezaji wenzake, wakiwa nje na ndani ya uwanja, anaona atapachika mabao mengi na kuvunja rekodi alizoziweka Cameroon akiwa na Dynamo Douala, kabla ya kwenda USM Alger ya Algeria.

"Nimeanza soka langu Tanzania kwa amani na furaha, mechi ya kwanza tu kucheza nimefunga, tena nimefunga dhidi ya timu kubwa, timu ngumu, Al Hilal, nitaendelea kufanya mazoezi kwa bidii, nitaendelea kujituma ili kuweza kushinda mchezo wetu wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli, kwenye mchezo huo nitakuwa vizuri zaidi ya mashabiki walivyoniona katika mechi dhidi ya Al Hilal na tutafanya vema," alisema straika huyo aliyesajiliwa badala ya raia wa Ivory Coast, Freddy Michael.

Ateba, amewaahidi wanachama na mashabiki wa timu hiyo, kufunga mabao mengi zaidi, kwani ndiyo kazi yake iliyomteta Tanzania.

"Naahidi nitaendelea kufunga mabao mengi zaidi na zaidi nikiwa na Klabu ya Simba, najua mpira si mchezo rahisi, lakini nimekuja hapa kutafuta matokeo, ninakuwa na furaha nikifunga bao, lakini kama Simba ikishinda mechi ni-

INAENDELEA UK. 23



Ateba

## Stars na sababu za kuiua Ethiopia leo kufuzu Afcon

**Faustine Feliciane na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Timu ya Taifa ya Tanzania ,Taifa Stars', leo kinaanza kampeni ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025, kitakapocheza dhidi ya Ethiopia huku Kaimu Kocha Mkuu, Hemed Morocco, licha ya kuweka wazi kuwa wamejiandaa na wapo tayari kwa mchezo huo, lakini pia akitoa sababu kwa nini ni muhimu kwao si tu kushinda bali kufuzu fainali hizo.

Stars itawakaribisha Wahabeshi hao kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanzia majira ya saa moja usiku huku ikiwa na lengo moja kuu la kuanza na ushindi nyumbani katika harakati hizo za kuwania kufuzu AFCON 2025.

"Tumejiandaa vizuri, ni mchezo muhimu sana kupata matokeo nyumbani, kushinda mchezo wa kwanza kutazidi kutuongezea kujiamini, nashukuru Mungu wachezaji wote wapo vizuri na kila mmoja anautaka mchezo huu," alisema Morocco.

Aidha, alisema wanakutana na Ethiopia leo huku wakiwa hajwakutana kwa muda mrefu na hiyo itaongeza ugumu wa mchezo huo, lakini wapo tayari kupambana.

"Wapinzani wetu tupo nao Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, lakini ukweli hatujakutana nao muda mrefu, tunajua wana kikosi kizuri na wameimarika zaidi, wanacheza kitimu, lakini sisi

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >